KUSOMEA CHINI YA MTI MUM (Muslim University of Morogoro) NA UCEZ(University College of Education Zanzibar)

Kisa changu cha kushindwa na kufaulu kusoma vyuo vya elimu ya juu ni kirefu. Lakini kutokana na majonzi niliyonayo nitasimulia kwa kifupi tu.

Katika maelezo ya kisa hiki nitasimulia kwa kuanza na hoja dhaifu ninazoamini zimechangia kulazimika kwangu kusomea chini ya mti vyuo vikuu. Mwishoni nitataja hoja na mapendekezo ambayo yangekuwa suluhisho la kuendelea kwangu na wenzagu na masomo hayo.
Wasomaji wa kisa hiki naomba tukubaliane kuwa mfumo wa elimu yetu, Tanzania bado umejikita katika kupima uwezo wa wanafunzi kukariri majawabu vizuri na kufaulu mitihani.
Kwa sisi ambao tulisomea A-level kwenye shule zilizoanzishwa kwa haraka za malengo ya kisiasa tuliathirika sana.
Shule yetu ilikuwa na vitabu na vifaa vya kutosha vya maabara lakini haikuwa na walimu kwa ajili yetu na wala uzoefu wowote wa kidato cha 5/6, hatukuwa na hata karatasi za mitihani iliyopita na wanafunzi wazoefu wa juu yetu kutusaidia kukariri majawabu.

Mambo haya yalipelekea kumaliza miaka 2 katika daraja la tatu, chini kwa daraja 2 kuliko nilivyomaliza kidato cha 4,katika daraja la 1. Maombi yangu mlimani (UDSM) na **SUA** hayakufanikiwa.Nilidhani kwa vile sikuwa na "**Combination**". Nililaumu somo moja ambalo tulilazimika kulisoma kisiasa.Hata hivyo wenzangu wengine waliokuwa na daraja la 3 kama la kwangu walichaguliwa.

Nikaitwa kufundisha, kuziba pengo la walimu kwenye shule ya sekondari mjini petu. Baada ya miezi mitatu nikachaguliwa kuchukua kozi ya Diploma ya Ualimu.Mwaka **1988** nilimaliza mafunzo hayo na kuanza kazi ya uwalimu rasmi.

Baada ya miaka takriban kumi na mbili ya kufundisha kwenye shule tatu tofauti za sekondari Pemba na Tanga, hatimaye mwalimu wangu mkuu akanipendekeza kujaza fomu za chuo kikuu cha Ualimu cha Zanzibar kilichomilikiwa na Africa Muslims Agency, shirika ambalo nilikuwa nikilifanyia kazi mwaka huo. Bila shida jina langu likarudi limechaguliwa.

Mwaka 2000 nikaanza masomo kwenye chuo hicho kilichopo eneo la Chukwani Zanzibar, wakati huo chuo kilikuwa bado kwenye hatua za usajili kuwa chuo kikuu kwa vigezo vya Tanzania.

Kabla ya kusafiri kwenda masomoni shughuli zangu za kibiashara ambazo nilikuwa nikijisaidia baada ya wakati wa shule badala ya"tuition" nilidhikabizi kwa mdogo wangu. Alikuwa ndio kwanza amemaliza masomo ya dini ya kiislam kiwango cha thanawi

Familia yangu nikaitafutia nyumba ya kukodi ya sehemu ya pekee isiyo na mchanganyiko wa wapangaji wengine.
Aliyekuwa mwajiri wangu alianza kubadili ahadi ya ufadhili wa masomo. Mwenyewe nikajilipia kila gharama iliyohitajika na kuanza masomo. Fani pekee ya masomo iliyonivutia ni "Islamic Studies" kinyume na masomo ya sayansi niliyokuwa nkifundisha sekondari.

Kuna ndoto ambayo tangu nlilipomaliza masomo ya kidato cha sita huwa inajirudia mara kwa mara usingizini mwangu. Mpaka sasa haijawacha kujirudia rudia katika sura tofauti tofaute za kindoto. Kama kwamba sikumaliza kujibu maswali kutokana na kuutumia vibaya wakati uliopangwa.

Ndoto hiyo pamoja na kisa cha Kaaab bin Malik daima imekuwa dira ya kuniongoza kuepuka uzembe na ajizi ya kutekeleza mipango yangu. Kwa hali hiyo mahudhurio yangu kwenye vipindi vya masomo na ratiba nyengine za chuo sikukubali kutawaliwa na aina yoyote ya uzembe. Nilijihisi kumudu vyema masomo yangu. Nilifurahia mijumuiko na wanafunzi wenzetu wa kutoka mbali. Mwaka huo tulikuwa na wageni wengi kutoka Ethiopia, Somalia na Eritrea.

Mwalimu wetu wa somo la "FahmulMasmuu" marehemu Mohammed Majid nakumbuka alivutiwa na jitiahada zangu pamoja na kwamba sikuwa na msingi wa fani hiyo kama wale wenzetu waliotoka vyuo vyengine vya Kiislamu.

Juhudi za walimu wa kisudani katika kazi na uwezo wa kufahamisha mada zao ulinichangamsha sana. Sitomsahau Dkt Skh Alwan na Ustadh Adam kwa uwezo wao wa kufundisha lugha ya kiarabu kupitra Qur'an, hadith na visa vya kweli badala ya paukwa pakawa. Tofauti kati yetu kama wale waliotokea vyuo vya kiislamu haikuwa ya kukatisha tamaa.

Matatizo upande wangu yalianza muda ambao tayari tulikuwa tunajitayarisha kufanya mtihani wa "Semester: ya mwanzo. Nilipokea simu kutoka nyumbani kwangu kuhusu tishio la kuporomoka kwa biashara yangu, ambayo ni wazi, ndiyo iliyokuwa inisomeshe na kutunza famila yangu. Hili sikulipa uzito mkubwa kutokana na furaha ya masomo. Niliazimia nisome kwa tabu ambazo nilizishuhudia wenzangu wengi wa kipemba na kiunguja tayari wakipambana nazo, kwa moyo wa kutokuridi nyuma.

Muda si mrefu tena, nikapokea simu nyengine wiki ileile,kuhusu kuvunjwa kwa makubaliano ya upangaji na bwana aliyetupangisha. Bili ya mazungumzo hayo ilikuwa ndiyo kubwa pekee niliyowahi kupokea ya simu yangu ya ya shirika la T.T.C.L. Kinyume na tulivyokubaliana..Mwenye nyumba huyo alilazimisha atumie chumba kimoja ambacho wakati akitupangisha alisema ni stoo. Alikuwa akitumia chumba hicho na marafiki zake. Siku chache alizoweza kutumia chumba hicho alikuwa akirudi nyumbani hata saa nane za usiku, na wa kumfungulia ilibidi awe ni mke wangu na shemeji zangu.

Hali hii ikanilazimisha kuondoka siku iliyofuata kwenda kutatua suala hilo la kimakazi. Nakumbuka nilivyopanda kwenye meli usiku huo huku machozi yakinitoka. Uzito wa shughuli iliyonifanya nirudi Tanga ulinifanya nisiweze kurudi chuoni mapema kama nilivyokusudia.

Ufumbuzi wa tatizo hili ulikuwa mzito, uliohitaji muda mrefu, Kasoro ya ushughulikiaji wa biashara kipindi tulipokua chuoni nayo nikajipinda kuirekebisha. Pirika za vitu viwili hivyo zikanimeza kimawazo mpaka nikashindwa kutekeleza ushauri wa Ibnu Ammi wangu ambaye nilimuacha chuoni akiendelea, kuhusu kuomba uakhirisho wa masomo.

Biashara ilikwenda vyema baada ya mwaka nikafanikiwa kupata ufumbuzi kwa namna fulani juu ya tatizo langu la kimakazi. Muda nao ukaenda mbio mpaka nikazinduka tena mwaka 2005 kutaka kurudi tena masomoni.

Wakati huo kulikuwa kuna matayarisho kabambe ya kufunguliwa chuo kikuu kipya cha kiislamu cha Morogoro (MUM). Pamoja na hamu yangu kubwa ya kutaka kuendelea na masomo lakini nilipendelea zaidi kusomea chuo cha karibu na nyumbani kwangu. Kwa hilo Morogoro niliona ingekuwa jibu la uchaguzi wangu. Nilipoona tangazo la kuanza kwa chuo linachelewa niliamua kurudi Chukwani kuulizia iwapo ningerushusiwa kurudi darasani.

Wahusika wa ofisi ya usajili wa wanafunzi. Kwanza walitaka kujua ikiwa nilikuwa na barua ya uakhirisho. Kwa vile sikuwa nayo niliwaonesha kitambulisho changu na risiti za malipo niliyokuwa nimefanya. Walisisitiza kuwa orodha ya wanafunzi wapya ilikwishatolewa na wakanishauri kuomba upya mwaka 2006.
Ushauri wa kuomba upya uliambatana na tahadhari kwamba uchaguzi wao kwa sasa sio kama ule wa 2000. Ni lazima kwanza upitie wizara ya elimu ya juu, kupata uthibitisho Dar-es-salaam.

Siku zilezile tangu nirudi Zanzibar kuulizia nafasi yangu ya masomo. Tangazo la kuanza chuo kikuu cha Morogoro likatolewa. Fomu za maombi zilitajwa zingetolewa kwenye ofisi za MDF jijini Dar-es- salaam, kwenye internet, Zanzibar na Chuoni Morogoro.

Ilipofika tarehe ya kuuzwa fomu hizo mimi nilikuwa wa mwazo kufika kwenye ofisi ya MDF jengo la kitega uchumi la NIC Dar-es-salaam.Mule ofisini nilikuta chumba kiko wazi lakini hakukuwa na muhusika yoyote. Mlinzi akanieleza ametoka, akanionesha kiti ili nikae kumsubiri.

Baada ya kumsubiri akafika kijana mmoja mrefu akiwa amepangatia bahasha ambazo nilijuwa ndizo fomu zenyewe nilizokuwa nikizisubiri, Akaniambia nizidi kusubiri kidogo kwani bado alikuwa akisubiri kitabu cha risiti cha mauzo cha Chuo. Mawasiliano ya simu aliyokuwa akiyafanya yalimfanya abadili mawazo ili anisaidie kuondoka mapema. Akaamua kutumia kitabu cha kawaida cha risiti ambacho kilikuwepo ofisini na angepiga tu muhuri wa chuo.

Akagundua hakuwa na karatasi ya kopi"Carbon paper" akanitaka nimsubiri tena kidogo ili akanunue madukani pale chini ya jengo lile la ghorofa nyingi lenye vichochoro vya giza. Hatimaye nikalipia na kuondoka na fomu zangu. Nikazituma haraka kwa njia ya rejista ya posta kutokea posta ya Ngamiani Tanga. Nikasubiri matokeo kwa shauku kubwa.Yalipotolewa jina langu halikuwemo. Sikuamini matokeo nikajaribu kuwasiliana na chuo kujua iwapo kweli fomu zangu zilifika nikiwa na shaka ya usafiri wa posta. Kawaida barua za rejista huwa zinarudisha kadi inayoonesha kupokelewa kwa barua ilikopelekwa, sikuwahi kupokea kadi hiyo.

Majibu ya simu niliona hayatoshelezi kila nilipotaka niunganishwe na wahusika wakuu, ilichukua muda mrefu wa simu kabla ya kufikiwa kwa aliyekusudiwa. Nikaamua kusafiri

mwenyewe hadi chuoni siku ya pili yake. Katibu muhtasi akanipeleka kwa bwana Tamimu. Naye akaniunganisha na makamu mkuu wa chuo, profesa Issa Musoke.

Kwa wakati ule ilionekana baadhi ya wanafunzi waliochaguliwa hawakuripoti na tayari masomo yalikwishaanza. Nikatakiwa niandike barua tu ya kawaida ya maombi. Nikapatiwa karatasi na kwa kalamu yangu nikaandika barua fupi ya ukurasa mmoja. Katika barua nikakumbusha vitu ambavyo niliviainisha kwenye fomu nilizozijaza kabla, kwamba niliwahi kuwa mwanafunzi Chukwani na kuwa nakusudia kujilipia masomo mwenyewe.

Pamoja nami,kulikuwa na watu wa aina yangu, ambao ni wazi walikuwa ama hawakuchaguliwa au walichelewa kuomba kutokana na muda kuwa mfupi. Tofauti na mimi, wao walipewa fomu nyengine za kujaza tayari kujiunga na chuo. Nikawaacha kwenye mabenchi wakijaza kwa furaha na mimi nikaenda kwenye chumba cha msikiti kusali sala ya Ijumma ambayo tayari ilikuwa imewadia.

Nilipoingia msikitini nikakuta khutba ikiendelea huku mmoja ya wanafunzi akiwa mbele anamalizia khutba ya mwanzo. Kwa barua yangu nikawa nasubiri kuitwa kupitia nambari yangu ya simu na anwani yangu ya barua pepe ambavyo kila mara tulitakiwa kuorodhesha. Sehemu ile nilijua ndiyo ingekuwa pahala pa kutolea misimamo thabiti ya kiislam juu ya masuala mbalimbali ya kijamii yatakayojitokeza kuhusu jamii ya kitanzania na ulimwengu kwa jumla. Sisi wanafunzi wa "Islamic studies" tungekuwa ndio tegemeo la wanafunzi wenzetu pale chuoni na dira kwa watanzania wenzetu.
Hamasa za siku ya zamu yangu kuhutubia zikanipeleka mbali, mpaka kuwawazia wanafunzi wenzetu wa kiislamu wa chuo cha kilimo cha SUA.

Wakati nimo garini kurudi Tanga bila mategemeo ya uhakika, nikawa napima jinsi waislamu wa Tanzania watakavyokuwa wakitegemea tafiti zetu. Nikawa tayari nina changamoto kwa wanafunzi wa kiislamu wa SUA. Waislamu siku za Ramadhani wanapenda sana futari ya mihogo, lakini mara nyingi wanagundua chakula hicho hakiliki kwa uchungu baada ya kuwa wamegharimika kukipika, kwa nini wa SUA wanashindwa kutafuta kitu kama "Litmus paper" ambayo ingetumika kugundua sumu ya muhogo katika hatua za mwanzo za upishi ?.

Siku chache baada ya kurudi Tanga nikaletewa matangazo mengi ya ufunguzi wa Chuo, shughuli ambayo ingefanywa na rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzaninia wa wakati huo; Benjamini Williama Makapa. Pamoja na kadi za mialiko nikawa nikiyasambaza na kutafuta wenzengu kunisaidia kwa furaha.
Wiki moja baada ya sherehe ya ufunguzi wa chuo, likatokea tangazo jengine kwenye gazeti.Tangazo liliwataka wale walioomba kwa kujilipia masomo, wafike chuoni na kila kitu chao tayari kwa kuanza masomo.

Kama kawaida yangu, siku iliyotajwa nikawa wa mwanzo kufika chuoni ukiondoa wenzangu wachache wa kutoka Dar es Salaam. Nilipotua mizigo yangu na kumlipa mwenye teksi, nikakuta hali ni tofauti na nilivyodhania. Hasa kwa upande wangu. Huku

wengine wakijaza fomu za kuhakiki mlo na malazi yao, mimi nikatakiwa nisubiri maelekezo zaidi.

Bwana Tamimu wa MDF chumba no. 5 akaliitisha faili la maombi yangu lililokuwa na jawabu la Makamau Mkuu wa Chuo kuwa niombe tena mwaka 2006. Pamoja na jawabu hiyo akaniunganisha na wahadhiri wawili wa masomo ya Islamic Studies na Lugha ya Kiarabu ili wanipe maoni na ufafanuzi wao kwa vile mule katika jalada haukukuwa na sababu za kuonesha upungufu uliolazimisha kuomba tena. Baada ya muda mrefu wa kuwasubiri watoke darasani wakafika na kuniita ofisini kwao.

Wote wakasisitiza kuwa huo ndio uamuzi wa mwisho na hawakuwa na namna nyengine ya kunisaidia. Wakanishauri ni vyema nifanye mtihani mwengine wa A 'level kabla ya wakati huo kwani matokeo ya mtihani huwa pia yana "expire". Wakaongeza kuwa chuo kina utaratibu mkali wa usajili wa wanafunzi na hata wao walimu. Wakasema ni lazima iwe hivyo ili kufuata viwango vya kimataifa. Nikaondoka mnyonge kurudi nyumbani na kwa upole nikawaahidi, ningetekeleza ushauri wao.

Kwenye gari nikakaa na ustadh mmoja rafiki yangu wa Dar es Salaam, ambaye mwenyewe alikuwa anasomea shahada ya juu Mlimani (UDSM) na ambaye alikwenda chuoni kumpeleka jamaa yake aliyemuacha huko baada ya kufanikiwa kumpatia nafasi. Nikatafuta maelekezo zaidi ya kutekeleza ushauri wa walimu wangu. Kwa kweli muda uliobaki kujisajili kwa kidato cha sita ulibaki mfupi.

Niliahidi kutekeleza lakini bado sikuwa na imani kamili na ushauri huo. Nikashughulishwa na majukumu mengi ya kimaisha mpaka muda ukaisha kabisa na muda wa kujaza fomu nyengine za mwaka wa pili wa masomo wa MUM ukawadia.

Masharti yaliyotajwa kwenye fomu hizo ya kufaa, kwanza kuuziwa tu hizo fomu, pamoja na kutofanya mtihani wa kidato cha sita niliona bado sifa hizo ninazo. Mwaka huu nilikwenda kulipa Sh. 20,000/= pale pale chuoni, nikajaza fomu pamoja na viambatisho vyote vilivyo takiwa. Aliyeniuzia formu alishangaa kwanini nisingejaza "Direct Entry" moja kwa moja badala ya "Mature age" niliyochagua. Mshangao wake ulitoa matumaini ya kutokuwa na shaka juu ya kutimiza masharti hayo.

Tangazo na fomu za maombi yalisema mtahiniwa kwenye mtihani wa mahojiano angepimwa pamoja na mambo mengine; uwezo wake wa ufahamu wa lugha ya kiingereza. Kuhusu kiingereza nilijiona kama tayari nimefaulu mtihani huo; kwenye kipengele cha Ufadhili wa masomo nilijaza nitajilipia mwenyewe.
Macho na fikra zangu yalikuwa yakisubiri muda wa kuchukua fomu za chuo cha Chukwani. Hivyo sikutulia Tanga. Muda ulipowadia nikawa miongoni mwa wa mwanzo kufika ofisi za AMA Tabata Dar es Salaam. Siku zile zile nilikuwa na safari ya kwenda Zanzibar, hivyo nikapendelea kurudisha fomu zangu za maombi kwenye ofisi za chuo mkono kwa mkono.

Nikiambatanisha na nakala za usajili wangu wa mwaka 2000 nikazikabidhi kwa wahusika ofisini. Ofisi ya University College of Education – Zanzibar (UCEZ) wakazipokea fomu

hizo kwa mikono mikunjufu. Kwa kuzipitia haraka wakanitoa wasiwasi wa kutochaguliwa na kwamba kuanzia hapo nijitayarishe tu na masomo kwani waliona nimetimiza masharti yote na zaidi wakataja cheti cha usajili kuwa kingekuwa cha msaada wa uhakikia.

Mazungumzo pale ofisini yalikuwa yananihakikishia nafasi ya masomo, mwakani, hata hivyo sikuamini maneno yale bila kuona ukweli wake kivitendo. Hivyo nikaazimia kuendelea na juhudi zaidi za kutaufuta nafasi hiyo kwenye chuo kikuu cha Morogoro.

Pale nje wakati nikitoka ofisi za msajili, nikakutana na mwanafunzi niliyefahamiana naye ambaye alikuwa katika safu za Uongozi wa wanafunzi Chuoni. Katika kujieleza kilichonipeleka pale na baadhi ya sifa zangu naye akanipa moyo zaidi wa kuchaguliwa, halafu akaongeza "Labda watumie uchechenia ndio watakuacha". Nilipotaka kujua zaidi kuhusu huo uchechenia, uliokuwa msamiati mpya kwangu, akaniambia ni Upemba kwani jambo hilo alisema lipo.

Kabla kutoka kwenye eneo la chuo, nikaamua kwenda kuchungulia jengo la kisasa la maktaba, moja ya majengo yaliyoongezekaa tangu mwaka 2000. Mule ndani kulikuwa na wanafunzi wachache, nikajiona kama kwamba na mimi ni mmoja wa watumiaji wake mwaka wa masomo ujao. Nikaondoka kusubiri tarehe ya mtihani.

Wiki moja kabla ya tarehe 18 march ya mtihani wa MUM likatolewa tangazo la kuakhirishwa kwa mtihani huo mpaka mwezi April. Mtihani wa April nao ukaakhirishwa kwa mara ya pili. Tangazo la uakhiriso wa pili halikutoka mapema, hivyo watahiniwa kama mimi tulikuwa tumefika kituoni siku moja kabla. Nilipojuwa hivyo nikatafuta sehemu ya kulala pale mjini na asubuhi yake nikarudi nyumbani. Mabadiliko hayo kwa upande mmoja niliona kama kwamba ni ya kheri kwangu kwani yalizidi kunipa muda wa matayarisho kitu ambacho nilijikaza nacho kila siku usiku wa manane.

Mahojiano ya chuo kikuu cha Chukwani yalifanyika kama ilivyopangwa mwezi Mei. Mimi na waombaji wengine kutoka bara tulifanyia kwenye kituo cha Tabata. Waombaji hawakuonekana kufikia hata sitini. Majibu ya kuandika yalikuwa ni kwa ajili yetu tu tulioomba kusoma "Islamic studies".Chumba kidogo tu cha ofisi kilitosha, wakati huo huo wenzetu wengine wakiitwa na kufanyiwa mahojiano ya mdomo.

Niliridhika na nilivyojibu mtihani ule kwa lugha ya kiarabu kitupu. Ukiondoa maswali mawili ya mwisho yaliyopima ufundi wa ziada wa kilugha upande wa Nahau na Swarfa maswali yaliyobaki yalipima uelewa tu maelekezo kwa lugha ya kiarabu. Niliporudisha majibu kwa msimamizi nilipata matumaini mazuri zaidi.

Aliopoona cheti cha usajili cha 2000 alichokuwa nacho kwenye fomu alizozipekua kunitambua alisema "Kumbe una cheti hiki! Kitakusaidia.

Tangazo rasmi la kuakhirishwa kwa mtihani wa MUM hadi June lilipotoka lilitoa tarehe kuwa ni tarehe 10 mwezi huo. Ilielezwa kuwa tarehe hiyo ingekuwa kwa watahiniwa wote wa *Mature age* na *Direct entry*. Fununu iliyokuwepo kuhusu kuakhirishwa kwa mtihani huo mara mbili ni kuwa kulikuwa na uchache mkubwa wa walioomba. Kwa upande

mwengine chuo kilikuwa kimetega kupata maombi zaidi kutoka kwa wanafunzi waliokuwa wamemaliza masomo kidato cha sita kwa mitihani ya March na April.

Juni nane simu yangu ikanikumbusha kwa safari siku iliyofuata. Mapema Juni 9 nikaanza safari hiyo. Jua lilipopinduka upande wa magharibi nikawa tayari nipo chuoni. Kitu cha mwanzo ilikuwa ni kuangalia jina na namba yako ya mtihani. Anayeona jina lake aelekee kwenye ukumbi kusubiri maelekezo mengine. Nambari yangu ilikuwa ni M11.

Kwenye ukumbi nilichagua kiti cha maeneo ya katikati kilichogandamizana na ukuta.

Nikakaa kimya kimya. Halafu nikatoa simu yangu nikawa naendelea na biashara zangu Tanga na Dar –es- Salaam. Mara moja moja nikawa nikiinua macho yangu kuangalia ongezeko la watahiniwa na uchangamfu wa vijana waliomaliza kidato cha sita ambao hawajaonana tangu wamalize mitihani miezi michache iliyopita.

Baada ya karibu saa nzima ukumbi ambao nakisia ulikuwa na nafasi ya kukaa watu mia tano ukawa umejaa wengine wakiwa wamesimama baina ya mistari na bado watahiniwa wakimiminika.

Nilivutiwa na mtahiniwa mmoja ambaye alifika na mtoto wake mchanga.Muda ule wa kusubiri akimnyonyesha kwa chupa motto wake, huku mkono mwengine akishikilia kalamu na vifaa vya kufanyia mtihani.

Takriban baada ya alasiri muhusika akafika na orodha zake na kukaa kwenye nafasi moja mbele ya ukumbi. Akaelekeza mmoja afike pale mezani kwake ataje jina na namba yake ili yeye amtajie sehemu ya kufanyia mtihani kesho yake; akianza na walioko mbele yake.

Kwa vile milango ya kuingilia ukumbini ilikuwa kule mbele, hii ilikuwa na maana sisi tuliofika mwanzo na kukaa misitari ya nyuma na katikati tungekuwa wa mwisho kuondoka. Magharibi ilikuwa inasogea kwa kasi na baadhi yetu tulikuwa bado kuswali.Wengine ambao huwa wepesi kueleza hisia zao wakaanza kushutumu mpango ule wote mzima. Kila mmoja akitoa fikra nini kingefanyika.

Punde likaanza sokomoko, walio nyuma ikawa wanasogea mbele.

Wenyewe kwa wenyewe watahiniwa wakajaribu kujipanga kwenye foleni. Hata hivyo waliokuwa ndio kwanza wanafika walijipenyeza na kuwahi kuondoka. Mpaka nilipokuwa naondoka mimi mtoaji namba na kituo alikuwa ameinamia karatasi zake na hakukutolewa utaratibu wa ziada kurekebisha hali ile.

Mimi nilipangiwa kufanyia mtihani shule ya "Foresthill", ambayo ilikuwa nje kidogo ya mji wa Morogoro kuelekea milima ya Uluguru. Nikafuatana na mwenzangu mmoja, ambaye katika mazungumzo tukafahamiana ana asili ya Tanga na anaishi Arusha. Punde tukawa marafiki na kusimuliana kila mmoja wetu shughuli anayofanya, na jinsi alivyofikia mpaka kuchaguliwa kufanya mtihani kesho yake. Kama mimi na yeye alikuwa amejaza fomu za "Mature age".

Kwa vile mimi sikuwa na mwenyeji pale mjini kama rafiki yangu, ikanibidi niende tena nyumba ya wageni niliyofikia mara ya pili mtihani ulipoakhirishwa. Baada ya kupata chumba nilichukua jukumu la kwenda kuona kituo chetu cha mtihani nikimuwakilisha mwenzangu, ambaye pamoja na kuwahi kuishi muda mrefu pale mjini alikuwa naye hapajui.

Nikaamua kutembea kwa miguu baada ya kujua kuwa eneo lile la "Forest hill" halikuwa na gari za abiria za daladala. Wakati magharibi inaingia ikawa nimefika na kupaona. Ushahidi ilikuwa nI bango la kuonesha kuwa ni kituo cha mtihani. Wenzetu wengine walifika na teksi na kupindisha kurudi mjini.

Siku ya mtihani ilipofika kwa wenyeji wa mji wa Morogoro lazima walihisi kufikiwa na ugeni mkubwa wa watahiniwa. Vikundi vya vijana wawili wawili na zaidi, wake kwa waume kutoka Tanzania nzima vilijaza mitaa na barabara iendayo kwenye vituo vya mitihani vya MUM.

Ukumbi ambao ulikuwa mkubwa zaidi ya ule wa Chuoni ulijaa, pamoja na vyumba vyengine viwili vya madarasa ambavyo vilikuwa vikubwa zaidi ya mara mbili ya madarasa ya kawaida.

Sikuwa na uhakika wa watahiniwa wenzetu vituo walivyopangiwa. Hata hivyo kwa kuangalia ukubwa wa ukumbi wa chuoni na pale "Forest hil" naamini sote kwa pamoja tulikaribia watu elfu moja na mia tano.
Mtihani ulikuwa ni kijitabu kilichokusanya maswali 150 yaliyohusu mchanganyiko wa masomo ya aina zote. Kwa mchanganyiko uliokuwa naamini hakuna aliyekuwa na uwezo wa kupata angalau asilimia tisini. Kwa sababu aliyejua sana Fizikia, Hesabati na chochote cha "0"level hakuweza kujua jina la Uwa la taifa la India.
Aliyejua jina la mtu anayevaa vazi kubwa jeupe na kufuga ndevu, basi lazima alishindwa kujua madhumini ya Marekani kwenda Iraki. Jee ilikuwa ni kuleta demokrasia au kutafuata silaha za maangamizi.

Utulivu ndani ya chumba cha mtihani kwa kiasi kikubwa ulikosekana, kutokana na ufafanuzi mwingi wa masuala ambayo ilikuwa wazi yamekosewa kuchapishwa. Maelekezo ya nini cha kufanywa pia yalitolewa kwa mdomo na wasimamizi.

Matatizo ya aina hii, wakati wa uwalimu wangu na usimamizi wa shule tulijaribu sana kuyakwepa kwa kuyarudisha kwa mtungaji au mchapishaji. Hii ni muhimu kwani suala lililokosekana halina jibu moja, na hivyo halipimi kitu chochoe kwa mtahiniwa.

Suala la mwisho la 150, niliona kama kwamba ndilo la kwetu sisi watu wa mahesabu. Kila nilivyoangalia umri wa Asha ukilinganishwa na wa Ali, haungeweza kuwa na jawabu mojawapo katika zile nne zilizoorodheshwa. Ilikuwa lazima liwe nijawabu la tungo. Ili kuwa mkweli wa nafsi yangu nikaandika "**No answer**", na haikuwa moja ya majawabu.

Fikra ya kufaulu mtihani ule,. Ilinijia zaidi pale nilipojihisi kung'amua kupata majawabu ya kifungu cha mtihani kilichokuwa na masuali karibu ya thelathini; ambayo hasa niliona ndiyo yaliyokusudiwa kupima uwezo wa kufahamu lugha ya kiingereza kama ilivyoahidiwa. Ilihusu kikundi cha ndugu kilichosafiri kwa ungo kuwahi kumuona mgonjwa masafa marefu, baada ya kukosa usafiri wa kawaida. Hata hivyo walipofika walikuta amekufa, lakini mmoja wao akamfufua.

Kabla muda wa mtihani kwisha kulitolewa tangazo kuwa kungekuwa na mtihani wa pili kuanzia saa 8 mchana. Ilikuwa ni tangazo lililowashutukizia wengi. Wachache waliamua kurudi makwao siku ile waliyoaga kurudi. Watahiniwa wa mfano wangu na rafiki yangu wa Arusha hutukuwa na haraka. Mimi ni karudi nyumba niliyofikia kurudisha begi langu na kuchua tena funguo.

Baada ya adhuhuri, wawili wawili na vikundi vikundi tukarudi kwenye mtihani wa pili. Tangazo jipya kabla ya kugawiwa mitihani lilitutaka tukae vyumba tofauti kati ya walioomba "Directenty" na "Mature age entry". Tulipokutana na wenzetu waliofanyia kituo kingine tulitakiwa tukae hivyo na kwamba hata idadi ya maswali ya kujibu ilikuwa ni tofauti.

Mtihani wa pili kilikuwa kitabu kikubwa kilichokusanya mitihani ya masomo maalum takriban kumi (10). Tatizo la asubuhi la makosa ya uchapishaji na maelekezo ya jumla lilijirudia.

Hata baada ya ufafanuzi mrefu bado kulikuwa na kugonga meza na mikono mingi iliyokuwa bado haijaelewa. Baadhi ya walimu waliokuja kusimamia safari hii walionekana kukerwa na jambo hili huku wakihamanika kupata ufumbuzi. Mhadhiri wangu ambaye muda mfupi tulisalimiana kirafiki alisikika akiguna huku akijaribu kuficha kukereka kwake.
Panapokuwa na ukosefu wa tahajia (spelling) kwa maneno ya kiengereza kawaida mimi huwa sinyooshi mkono, mara nyingi naelewa neno lililokusudiwa au maana ya tungo.

Hata hivyo nililazimika kutaka ufafanuzi wa idadi ya mitihani niliyotakiwa kufanya. Kufuatana na uchaguzi wangu wa mwanzo wa fani niliyopendelea kuisomea, ilionesha kama kwamba nilitakiwa nijibu mitihani mitatu, lakini karatasi ya kujibia ilikuwa na nafasi ya kujibia mitihani miwili tu. Kati ya masomo matatu nilitakiwa nifanye "Islamic knowledge" na moja kati ya Arabic au English. Niliamua kujibu "Islamic Studeis" Na Arabic.

Mtihani wa Arabic kama ilivyokuwa ule wa Chukwni haukukazia kwenye undani wa lugha. Ulipima uelewa wa mtahiniwa kufuata maelekezo ya jumla kwa lugha ya kiarabu ambalo lingekuwa msingi wa kuendea ufundi zaidi masomo yatakapoanza. Ukiondoa mwandiko wangu ambao si wa kuvutia kutokana na kulemaa kuandika kizungu niliridhika na jinsi nilivyozipanga upya tungo zilizoparaganywa kwa mfano mpangilio wa maneno ya mwenzetu mmoja aliyependelea kwenda kusoma Yemen.

Haikuwa tabu kujua aina ya mboga mboga alizokuwa akilima mkulima fulani na kuzipeleka mjini kwa gari lake la punda. Kwa upande wa Islamic ndio kabisa ulikusudiwa kuwatambua tu watahiniwa. Mazungumzo yaliyozagaa baada ya mithani ya jioni ni kuwa ilikuwa ni ya matumaini zaidi kuliko ule wa asubuhi.

Vijana wengi walitoka baada ya kumaliza hata kabla ya nusu ya wakati kwisha. Mimi nilikuwa kati ya wachache tuliotoka baada ya kumaliza hata kabla ya nusu ya wakati kwisha. Mimi nilikuwa kati ya wachache tuliotoka mwisho katika mitihani yote miwili. Nilihakikisha nilivyojibu ndivyo nilivyotaka na nilivyojua. Nilipata muda wa ziada kutupia macho mitihani mengine, kwa upande wangu hasa Fizikia na Hesabati. Pamoja na miaka mingi kupita sikuona mabadiliko yoyote ya vitu vilivyotahiniwa ilikuwa ni vilevile Matrix, Venn diagra, kuintergrate kuanzia a mpaka b n.k. Ndani ya fizikia sikuona vitu ambavyo viliashiria pengine wasomi wetu wako karibu kuleta ufumbuzi wa matatizo makubwa yanayoikabili nchi yetu kama vile umeme wa mgao.

Siku ya tatu kwa tuliotoka mbali, tukarudi makwetu kusubiri matokeo. Mwezi mmoja ulipopita bila jibu lolote wanafunzi wangu ambao tulifanya mthani pamoja wakaanza kuniuliza imekuwaje mbona kimya wakiamini mimi naweza kuwa na taarifa zaidi. Kwa upande wangu nilitumia kipindi hicho kumalizia marekebisho ya uendeshaji wa shughuli zangu wakati nitakoposafiri kwenda masomoni. Nilianza kazi hiyo mapema zaidi kuhakikisha kosa la mwaka 2000 halijirdii tena.
Kati ya wachache waliojua kuhusu nia yangu hiyo ya kurudia kusoma kishule walihisi mimi si wa kusoma tena wakisingizia majukumu mengi niliyokuwa nayo ambayoyalihitaji usimamizi wangu binafsi. Mmoja wapo ni ndogo wangu na mwanafunzi wangu wa mwanzo ambaye kwa sasa anasomea shahada ya pili mlimani. Alipoona huzuni yangu kubwa baada ya kulazimika kuondoka chuoni mara ile aliniahidi yeye angekuja kunishikia baadhi ya majukumu baada ya yeye kumaliza shahada yake ya mwanzo. Akanihimiza kutafuta ufumbuzi wa tatizo la makazi kipindi hicho.
Tulipokutana nyumbani Unguja wakati nikikimbizana na kujaza fomu kwa wakati uliopangwa, alikuwa na mawazo tofauti. Kwa hamu yangu ya kuendelea na masomo hasa kusomea Uislamu nilijifanya siambiliki. Hoja zote zilizotolewa za kunishawishi kutoendelea na masomo hazikunivutia hata kidogo, pamoja na kuona ukweli wa tishio la kuporomoka kiuchumi.
Dalili za kukaribia kutoka majibu ya kujiunganavyuo vikuu zilianza kujitokeza. Kwanza ilikuwa ni habari ya gazeti la AN-NNUR la Julai (7-13). 2006 iliyosema **HUU NI USALITI**. Katika habari hiyo lilitajwa baraza la vyuo vikuu la Tanzania, Tanzania Commisssion of Universities (T.C.U). Habari hiyo ilinukuu uidhinishwaji au uchaguzi wa mwanzo uliokwishakufanywa na baraza hilo. Ilinakiliwa idadi ya wanafunzi na vyuo vyao vingi vikiwa ni vile vinavyomilikiwa na taasisi za kikristo.

Habari ile ilinipa harufu mbaya ya udini wa baraza hilo, na ubaguzi wa aina nyengine. Kama nilivyowahi kuwa muathirika wa ubaguzi wa aina tofauti huko nyuma, mdudu huyo niliogopa bado ataniandama na kunidhuru. Nilihofu angeharibu uchaguzi wangu kwenye sehemu yoyote ya mchakato huo.

OSAMA NA WACHECHNYA WANAHUSIKA

Makombora ya mwanzo ya vita vya msalaba vilivyo anzishwa na Bush nchini Afghnistan yalirushwa waktai nimo garini katika misafara ya kutafuta riziki.

Wiki moja tangu krusedi hiyo kuingizwa Iraki pia ilinikuta nimo safarini upande wa Kenya kwa madhumuni hayo hayo. Jina la Osama lilikuwa limetawala vyombo karibu vyote vya habari.

Tulipopita kwenye kijiji kimoja huku mwenyewe nikiangaza huku na kule kufaidi mandhari za barabarani, mara kikundi cha vijana waliokaa barazani walipiga mayowe" Shusha Osama huyoo! Maneno yao hayo yaliashiria kutaka nishushwe pale na dereva ili wanipige kulipiza kisasi cha Marekani iliyokuwa ikimtafuta mtu huyo kwa udi na uvumba bila mafanikio.

ZOMBE ASEMA MIMI NI OSAMA.

Mkasa mwengine mkubwa ulinikuta mwaka 2000 baada ya ule wa kulazimika kukatisha masomo mnamo tarehe 25 mwezi Agosti vijana wa Zombe[1] walifika kwenye eneo letu la biashara wakitafuta jiko la TANALEC lililoibwa sehemu. Kwa mujibu wa hati ya upekuzi jiko hilo lilidhaniwa limefichwa dukani kwetu.

1.Zombe hivi sasa anashtakiwa kwa kutumia cheo vibaya na kuua wafanyabiashara wa madini na dereva wa teksi.

Upekuzi huo ulifanyika kwa kuinua vitu vidogo vidogo kama vitabu na madaftari. Mwishowe wakapata majarida ya zamani yaliyomtaja Osama na kuyaandikisha na kuondoka nami. Moja lilikuwa ni jarida la **FOCUS ON AFRICA** na vingine ni vijarida vya **MSAUD** na vya vijana wa Kiislamu Dar-es- salaam ambavyo havikuwa vimesajiliwa.

Tulipofika nyumbani walikuwa wamechoka kupekua kama vile walivyofanya dukani na usiku ulikuwa umekaribia. Ili kukamilisha ripoti yao walitaka kujua tu iwapo nilikuwa na vitu kama kadi na bendera za CUF.

Wazee wangu wengi wa Kipemba waliingia mtegoni na kushikwa wiki ile ile kwa kosa la kukutwa na makaratasi ya uchochezi, ambayo waliyapokea jioni moja yalipokuwa yakigawiwa eneo la stendi palipokuwa na maskani yao.

Siku hiyo ndipo baba yangu aliponililia kwa kwikwi wakati bado nipo hai. Ilianza kama utani tu mara baada ya adhuhuri, na hatua kwa hatua akawa hanioni mpaka nikatoweka machoni pake kabisa bila kupata kauli yangu, ya nini kilitokea.

Nilipofikishwa machoni kwa afande Zombe kwa mara ya pili usiku alin'gaka "Huyu Osama wa nini hapa? Anaweza akaj …….. Mrudisheni kule". Hapo ilikuwa ni saa nne usiku, sisi tukishuka ngazi na askari wake wawili masafa kutoka kituo cha polisi Chumbageni, walikonipeleka kunihoji zaidi.

Neno lake ambalo hakumalizia liliashiria kuwa ningeweza kujiripua, na pengine kuhatarisha maisha yao na kuharibu jengo la ofisi yao.

Nikarudishwa kwenye chumba kilichojaa washukiwa wa kila aina. Mmoja alikuwa ni mshukiwa wa ujambazi, ambaye alikuwa amevunjwa mguu. Kwa maelezo yake ni kuwa isingukuwa ni mmoja wa askari waliokwenda kumshika, ilionesha wenzake walipata amri ya kumuua kabisa. Usiku kucha alilalamika maumivu na mguu ulivimba huku akivuja damu bila hata aspirini.

Mule ndani tulikuwa wengi hata nafasi ya kujinyoosha sakafuni ilikuwa shida. Nakumbuka kulikuwa na vichaa wawili ambao muda wote walikuwa wakiropoka ropoka, na mmoja alikuwa ni muuwaji wa kutumia bunduki, ambaye alikuwa akisubiri taratibu za kumsafirisha kumpeleka Moshi. Tofauti na washukiwa wengine yeye hakukataa kosa lile na muda mwingi alirusha mikono hewani kinamna ya mapigano ya kareti.

MIMI SIMJUI OSAMA.

Si kwama nimefanana kweli na Osama, na wale wote wanaoniogopa si kwamba hawajui hivyo.Lakini hiyo ni kejeli ambayo imewapata wenzangu wengi, watu wenye chuki na ubaguzi hata sifa moja tu inatosha kuwatia homa ya maradhi yao.

Mimi nyumbani kwao Osama wala sikujui, iwapo tumefanana kwa baadhi ya sifa, basi bado tunatofautiana kwa mengi na kumfanya yeye awe ni tofauti na mimi.

Wengi ya wale wanaomchukia na kumuogopa Osama naamini wana uhusiano mwengine mkubwa kuliko mimi. Wengine wana sifa ya Utanzania kama sisi, lakini wanazungumza lugha moja na Osama, wameishi huko kwao Osama muda mrefu na kuzaa watoto huko huko. Kwa ubaguzi wa sura nyengine, wao ndio huchaguana peke yao kwenda kufanya kazi kwenye balozi za Tanzania huko; Ndugu hata mmoja sina huko.
Mmoja ya watu ambaye nimepambana naye akinishambulia kwa kauli za ubaguzi alikuwa na jina kama la kwangu. Siku moja niliamua kuchangia kidogo mjadala wa kisiasa uliohusu uchumi kwenye kikundi alichokuwapo. Hata hivyo alifanikiwa kuninyamazisha kirahisi aliponiambia “Nyinyi ndivyo mulivyo hivyo, basi pandeni meli na ndege muende kwenu huko!”

Mara nyengine hujiona mimi ni mpemba sana, lakini kuna wapemba ambao wanaposhindwa hoja hupata kipengele cha kuniita mimi ni mtu tofauti na wao.

Ninaposhiriki kwenye shughuli za kiuchumi na kupeleka maombi yangu mengine kwenye taasisi mbalimbali, hufanya hivyo kwa kujiamini kuwa mimi ni Mtanzania, lakini bado nahisi kuwa watanzania wenzangu ambao wananiona mimi mtu mwengine kabisa.

Kwa kipengele hiki cha hofu ya Osama na ubaguzi wa mtu atokeako, Wahadhiri na Wakuu wa vyuo vya MUM na UCEZ nawapa dhana nzuri ya uadilifu, na kwamba kwa utambuzi wa dini yao na usomi wao hawawezi kutumbukia kwenye mkorogeko wa upuuzi huu ambao kisomi hauna maelezo yaliyonyooka.

Nachukualia kwamba jina langu lilipita ama kwa sifa za Vyeti au kwa wote kunijua hima yangu ya kupendelea kuendelea na masomo. Tofauti na watahiniwa wenzangu wengi, katika kila jopo naamini kulikuwa na angalau mmoja aliyenijua nje ya chumba cha mtihani.

Sina maana ya kuchaguliwa kwa kujualikana kwa maana ya kupendelewa tu, lakini kwa sifa zangu zilizojadilika iwapo kulikuwa na vikao vya kufanya hivyo.

TATIZO NI T.C.U; KUNA MKONO WA FBI?

Tukiangalia majigambo ya taarifa zinazohusiana na vita dhidi ya ugaidi na uzoefu wa Marekani kujipenyeza bila haya kila pahala, si ajabu ndani ya T.C.U kukawa na wajumbe maalum wa FBI.

Agenda ya vita vya muda mrefu dhidi ya ugaidi ni pamoja na kupambana na elimu za waislamu. Vita hii inazuia watu fulani kusoma. Wale wanao soma wanazuiwa kusomea baadhi ya fani za kielimu. Wale waliosoma tayari elimu hizo basi wanatiwa vizuizini na hata kuuliwa.

Israel, Marekani na Urusi zimeuwa wataalamu kadhaa wengi wao wakiwa ni waislamu, ambao waliona elimu zao zinakwamisha nia zao za kuitawala dunia. Uingereza nayo imeingia kwenye mtandao huo wa kuogopa wasomi

Urusi kwa kushirikaana na Pakistani ilimuua Skh. Abdallah Azzam mwishoni mwa miaka ya 1990, alikuwa ni mwalimu na mtaalamu mkubwa wa fani za kiislamu mwenye asili ya Palestina, Israel imeua wataalamu wengi wa Kipalestina, mtaalum wa miripuko na maroketi, Yahya Ayyash ni miongoni mwao. Katika vita vya Israel na Lebanon vilivyositishwa hivi karibuni, Israel hiyo hiyo ilituma helkopta maalum ya kwenda kumuua mtaalamu aliyehusika na urushaji wa kombora la masafa marefu la Hizbullah, kwenye mji wa Bint Jubeil. Hata kama na wao hawakurudi nyuma lakini Israeli ilijigamba kwa kufikia lengo.

Mfano wa wazi kuwa wasomi wanaoogopwa na elimu zao ni tatizo, ni kuuliwa kwa kiongozi wa chama cha **HAMAS** Skh. Ahmed Yassir mwaka juzi. Pamoja na kwamba alikuwa mzee sana na hakujiweza hata kutembea kwa miguu yake, bado Israel iliamua kumuua kwa kutumia kombora kubwa la angani, alipokuwa akiotoka msikitini kwa Sala ya alfajiri.

Marekani lipoingia Irak kiujanja nia mbaya ya kuangamiza, ilishirikiana na Israel kuwaua na kuwafunga wasomi chungunzima. Wataalamu wanaoogopwa si wale wenye elimu za juu tu, hata wenye ujuzi wa wastani unaohitaji afya ya mtu na akili timamu tu ni hatari katika vita hivyo. Baada ya Septemba 11 ya 2001, vijana wanaokwenda kusoma Marekeni wanachunguzwa vya kutosha. Elimu nyingi vijana hao wanazuiwa wasizisome hata elimu ya kurusha ndege ni marufuku kwa wengi wao.

Mabomu yaliyoripuka Tanzania mwaka 1998, yameifanya nchi hii iwekwe mbele katika vita dhidi ya Ugaidi vya Marekani na washirika wake. Tanzania nayo imewawachia watu hao Uhuru wa kupenya sehemu yoyote waipendayo. Sehemu kama T.C.U ambapo ni

mapitio muhimu ya wasomi kwa utaratibu huu mpya, lazima kutawavutia wajumbe hao wa FBI.

Kwa hofu tu ambao mara nyingi zimegeuka kuwa za bure, Marekani inaweza isione haja ya kusubiri baadhi ya watu wasome halafu ndipo ije ipambane nao mapangoni. Hatua muhimu kwa falsafa zao ni kuwazuia wosisome ili wabakie wajinga na wasiwe na sauti zozote katika jamii.

Ukiondoa falsafa za vita dhidi ya Ugaidi, kuzuia watu kusoma au kuwapunguza idadi yao kuna faida kubwa kwa kundi lenye chuki dhidi ya kundi jengine. Hivyo katika tume za kuchagua nani asome kunaweza kukawa na watanzania wenzetu wanaotaraji kufaidika kwa kuwawekea vikwazo watanzania wenzao.

Katika orodha za waliochaguliwa kusoma MUM na UCEZ wamo wachechnya na akina Osama kadhaa, lakini hii haitoshi kufuta uwezekano wa wengi kuacha kuchaguliwa kwa vile kwanza hatujui ni wangapi walioomba nafasi hizo na wangapi hawakuona majina yao. Kama zilivyo tume nyingi za uchaguzi kuhoji matokeo mara nyingi kunaonekana ni ukorofi tu wa aliyekosa kura.

Kusaidia kujenga hoja ya kipengele hiki cha mjadala wangu tayari mpaka naandika makala hii nawajua waombaji wawili waliopeleka maombi yao kwenye vyuo viwili na wenye sifa za daraja la juu ambao hawakuona majina yao kote kuwili. Mmoja wao ana matokeo ya daraja la kwanza kidato cha Sita katika maosmo matatu ya lugha yenye A ya kiarabu. Yeye anamlalamikia mwenzake mkristo, ambaye ana daraja la tatu ambaye amechaguliwa kusomea fani ya masomo ambayo wala hakuiomba.

MZIZI WA FITNA WAKATWA.

Muda tuliokuwa tunasubiri matokeo kulikuwa na majadiliano yakiendelea mitaani miongoni mwa wanafunzi watarajiwa na kwenye vyombo vya habari; juu ya suala la mikopo ya Serikali kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu. Ilihusiana na nani anayestahiki kulipiwa na tume ya mikopo kati ya wengi wanaohitaji.

Nipashe liliandika "**Lowasa akata mzizi wa fitna"**. Habari hii ilimkariri Waziri Mkuu akitaja sifa kuu ya kulipiwa na Serikali kuwa ni kufaulu kwa kiwango cha daraja la kwanza au la pili kwenye mitihani ya kidato cha sita.

Kwa habari hii ikanipitia akilini mwangu kuwa vyuo nilivyoomba vingeifanyia kazi fitna hiyo ya pesa na kuacha kuzingatia sifa nyingine zote za waombaji ili kwa mtazamo wao waweze kuendesha bajeti zao kiuhakika.

Matokeo yalipotoka ya MUM kwenye gazeti la Annuur la Julai 28 yalidhihirisha hivyo kwa kiwango kikubwa. Jina langu wala halikuwemo.
Mwanafunzi wangu ambaye tulifanya mtihani pamoja kwa kuwajua wenzeke alinithibitishia hivyo.

Ipo shaka kuwa matokeo ya mitihani ya Juni 10 wengi wetu tuliyojikaza nayo sana wala hayakuzingatiwa. Hata ule uwezo wa mawasiliano kwa lugha ya kiingereza nao haukupewa umuhimu kama ulivyotangazwa kabla.

Nawajua baadhi ya waombaji ambao wana sifa nyingine bora lakini siku ya Juni 10 nilikuwa nikiwahurumia sana, lakini matokeo ya Julai 28 mambo yaligeuka na zamu ya kuhurumiwa ikawa yangu.

Kwa vile niko katika kutaradadi juu ya sababu iliyokatisha mbio zangu za kusoma sakafuni kwa kufikia ukingoni. Kwa faida ya wanafunzi watarajiwa walimu na wazazi nabadili msimamo ili nifahamike zaidi.

Katika mtazamo huo na kuzingatia fitna ya fedha, nachukualia kuwa tume za uchaguzi za MUM na UCEZ hawakunichagua kamwe, ma waliniona sifa zilizotajwa na Serikali sina. Kwa hali hiyo jina langu wala halikupelekwa kwa T.C.U kwenye mikono mingi yenye maslahi tofauti.

KWANINI SISIKILIZWI.

Kwa hofu ya pesa vyuo ninavyoviita vyetu vitakuwa vimeniwachwa bure. Kule Chukwani watakuwa wameona risiti zangu za malipo ya mwaka mzima ambao sikuumaliza, na wangetaka kujua ningewaambia tena nitalipa mwenyewe.

Kwa upande wa Chuo Kikuu cha Waislamu cha Morogoro niliwaarifu hivyo kwenye fomu yao.

HAKUNA MADARASA!

Tatizo yawezekana kwa vyuo vyote viwili ni ukosefu wa vyumba vya madarasa, wenye maana ya kutokuwa na nyenzo za kutosheleza kusomesha wanafunzi wengi.

Iwapo kweli wahusika wa vyuo hivyo walikuwa na nia ya kuwainua waislamu kielimu, kwa kuangalia uwezo wa wenzao kwenye vyuo vya taasisi za kikristo, basi wanaweza kupewa sifa ya kuzembea kazi.

MUM wamechukua wanafunzi 200 na UCEZ 288, ni idadi ndogo sana ikilinganishwa na tulioomba na ambao wengi wetu naamini tuna sifa za kuendelea na masomo.

Au tuseme ni mashinikizo ya T.C.U na tume ya mikopo ili kufikia viwango Fulani vinavyoitwa vya kimataifa.

<u>DARAJA ZA KUPASI ZINA KIINIMACHO</u>.

Ni kweli kuwa katika kufanya jambo lolote ni muhimu kuwa na vigezo vya kufuata ili kufikia malengo. Kwa upande wa masomo ya darasani ni kutumia mitihani.

Hata hivyo malengo na nia ya elimu yanafanya mitihani isiwe kama penalty za mchezo wa mpira wa miguu; mmoja akifunga wengine wanashangilia na muamuzi anatoa ushindi usiojadiliwa.

Sote wenye uzoefu wa uwalimu tunajua jinsi wanafunzi wanavyobadilika utendaji wao. Wengine hutoka kwenye upocho kwenda kwenye uhodari kwa kupewa ushauri mzuri na kumbadilishia baadhi ya mazingira yaliyoonekana kumuathiri. Wengine huwa ni kinyume chake kulingana na kukosa ushauri na kubadilika hali za hata kiafya mwilini.

Haina maana kuwa walio na daraja za chini katika matokeo ya mitihani ndio wa kutengwa tu na kupangiwa kufanya kazi Fulani Fulani masokoni na mitaani. Hakuna sababu ya kuwakwamisha kwa hoja ya kutaka viwango vya Kimataifa.

Tukija kwa malengo ya elimu kiislamu ndio kabisa, ni ibada hasa kuwasaidia watu kusoma kwa upande wa waislamu Tanzania, ambao tumebaguliwa kielimu huko nyuma; ni jukumu la vyuo vyetu kuwatafuta hata waliofeli kabisa kuwasaidia kusoma.

Ni muhimu wale walioshindwa kufaulu na kufikia daraja Fulani kupewa fursa tena wakitaka kufanya hivyo. Kushindwa kufikia daraja hizo si kipimo cha uhakika cha uwezo wa akili zao. Kama nilivyotaja kabla mazingira ya kusomea na hali za msomaji vina mchango mkubwa wa matokeo hayo.

Mimi mwenyewe nimemfundisha mdogo wangu ambaye kwa sasa anasomea shahada ya juu. Yeye naye mara ya mwanzo alikosa kuchaguliwa akapitia mzunguko mrefu uliomfikisha hapo. Wale aliowasindikiza mara ile kwenda mlimani walishindwa njiani ama tuseme walirudishwa kwa sababu mmoja wao aligoma kuzuiliwa kwenda kuswali.

Rafiki yangu mkubwa kidato cha sita alikuwa na kipaji cha kufahamu kisichokuwa cha kawaida na juhudi. Hata hivyo kutokana na mazingira yetu hakufaulu kwa daraja kubwa, wakati nilipomsindikiza kwenda Mlimani. Kule Chuoni alifanya maajabu, na kwa sasa ni profesa wa kutegemewa kwenye moja ya vyuo vyetu nchini.

Naye rafiki yangu wa Arusha mwanzo aliishia darasa la saba. Akasoma madrasa za taasisi ya Maawal Islami karibu na Chuda jijini Tanga. Alipokusudia kujisomea sekondari amefaulu vyema na asipowekewa vikwazo Inshaa Allah atafika mbali.

Hiyo ni mifano michache niijuwayo mimi, ambayo naamini inaweza ikawapa wakati mgumu kuitolea maelezo wale watafiti wa elimu na saikolojia ya makuzi ya binadamu.

MADARASA YA CHINI YA MITI.

Kulingana na mazingara na haja iliyokuwepo, kwa miaka mingi Tanzania kumekuwepo madarasa ya chini ya miembe na mizambarau ili kuwawezesha watoto wengi kupata angalau elimu kidogo.

Baadhi ya waliosomea madarasa hayo, wengine wamefikia mbali zaidi kimasomo na kimaisha, kuna ubaya gani kwa vyuo vyetu kufanya mpango huo ili kuwawezesha waislamu zaidi kusoma.

Kwa maana hii, vyuo hivyo vingetengeneza utaratibu wa kusomesha wanafunzi zaidi si lazima wote wakae kwenye mazingira ya chuo kama vile sekondandari zenye dakhalia.

Suala la pesa lisipewe sura, iliyopo sasa, kwamba ni muhimu pesa hizo zitoke tume ya mikopo. Ni kweli kuwa kusoma Chuo Kikuu ni gharama kubwa, lakini kuna familia zenye uwezo wa kuchangia masomo ya watoto wao kwa kila mmoja kutoa kidogo alichonacho, na wako matajiri ambao mamilioni ya fedha hizo wala si tatizo kwao. Tupo wengine ambao kwa haja ya kusoma kwetu, pamoja na kutokuwa na uwezo wa kutosha wa gharama hizo, lakini tumejipangia kusoma kwa namna za kujibana kimatumizi, tuna uzoefu wa hilo.

Vipi watu wa aina zetu tuwachwe tu kwa kutishwa na T.C.U na tume ya mikopo, kuhusiana na pesa na viwango vya kimataifa.

VYUO VYA KIMATAIFA VIKO WAPI?

Kushughulishwa na kuingia kwenye viwango vya vyuo vya kimataifa kunaweza kukatuzubaisha waislamu na tukatoa wasomi wasiokuwa na faida kwa taifa na jamii yetu.

Katika mtazamo wa kimataifa waislamu hawatakiwi kujua namna ya kurutubisha nyuklia wala kutengeneza makombora ya masafa marefu. Bila shaka hata kutengeneza vyombo vya kwenda anga za juu ni kwa ridhaa ya Marekani na nchi za Ulaya.

Mataifa makubwa hayo hata nini cha kusomeshwa mashuleni kuhusu dini pia wanalazimisha iwe ni kwa mtazamo wao. Sasa ikiwa vyuo vyetu vinakubali hali hiyo na kukimbilia kuwa watiifu vitakuwa havijawakomboa waislamu na watanzania kwa jumla.

Waislamu kwa ushahidi wa Iran, Iraq na Pakistani ndio wanaowekewa vikwazo zaidi kutumia teknolojia ya nyuklia, lakini hata wengine wasiotakiwa kutokana na misimamo yao wanapingwa kuwa na teknolojia hizo kwa mitazamo ya wale wanaoita vigezo vyao kuwa ndivyo vya kimataifa.

HATA MABABU WA KIKRISTO WANASOMA KWA PESA ZETU.

Kwenye fomu za maombi za UCEZ za 1999/2000 zilitaja umri kuwa usizidi miaka 35. Za mwaka huu sikuona kitu hicho, huenda wamezingatia maana ya elimu kwa mtazamo wa kiislamu, kwamba elimu haina mwisho wala kikwazo cha umri

Elimu pia si biashara, kwamba uliyesomesha lazima akutumikie ndio uone umefaidika kwa pesa yako. Kifo pia hakina uzee, kwamba msomeshaji anahofia kifo.

Ikiwa kigezo cha umri bado kinazingatiwa kisiri na vyuo vyetu, basi vyuo hivi vitakuwa ndio vitiifu zaidi na vimepitwa na vile vya Serikali na taasisi za Kanisa

Nilipokuwa narudisha fomu za moambi Chuoni kwenye daladala ya Darajani Chukwani nilibaki na dada wawili gari ikimalizia safari yake. Niliwajua kuwa ni wanafunzi wa Chuo kwa jinsi walivyojishughulisha kumaliza kazi zao mule mule garini kabla kuingia kwenye kipindi kipya.

Hatua chache zilizobaki kufikia lango la kuingilia Chuoni tulitembea kwa miguu pamoja. Baada ya kuamkiana nilitumia fursa ile kuwauliza mambo machache kuhusu chuo ambayo sikuwa na uhakika nayo. Nikataka kupata ufahamu wao iwapo bado umri wa muombaji unazingatiwa. Mmoja wao ambaye kwa msemo wake nilijua ni mzaliwa wa mangapwani au sehemu nyengine ya kaskazini ya unguja alisema "Hata mababu pia wapo wanasoma."

Mababu aliokusudia haiko wazi ni wale waliochaguliwa kabla ya TCU kuonyesha makucha yake au ni mababu wapya. Kama nilivyowajua wao, na wao wakanijua kuwa nilikwenda kurudisha fomu, wakataka kunifahamu zaidi. Baada ya kujieleza, mwengine akianiombea dua. "InshaAllah mwakani tuwepamoja." Naamini wangependa iwe hivyo. Lakini maamuzi hayo si yao.

Shughuli zangu za kutafuta maisha huwa zinanikutanisha kirahisi, na kila siku na wasomi au waombaji wa masomo wa vyuo vya elimu ya juu. Hawa ndio wanozingatiwa kwa ajili ya kupatiwa mikopo. Wamo wengi sana ambao ni wazee kuliko mimi; Zaidi ni kuwa kwa majina na mila zao karibu wote ni wakristo.

Kwa mambo mengi imani yangu inanisaidia kutokuwa mchoyo, lakini kwa mababu/mabibi hawa ninapowaona roho huwa inaniuma sana. Sababu kuu ya kuwa hivyo ni kuona kuwa wanafaidi pesa ambazo mimi binafsi nimezichangia.

> Fedha ambazo nimeshachangia Serikalini kwa zaidi ya miaka 15 ya biashara ni mamilioni ya fedha. Mchango huu ni kupitia kodi za mapato na VAT. Jumla ya fedha hizo zinatosha kunigharamia mimi mwenyewe na wenzangu kadhaa kusoma chuo chochote kwa kipindi cha miaka mitatu hadi minne.

Kwenye fomu za moambi za vyuo kungekuwa na sehemu ya kuonesha mchango wa fedha wa muombaji binafsi au familia yake katika pato la serikali, basi risiti na mchangonuo wa mahesabu ya mhasibu ambazo ningeambatanisha, namini katika orodha ya waliochaguliwa chuo chochote ningekuwa na nafasi ya juu.

ELIMU HAINA MWISHO

Asili ya elimu yoyote ni Allah(s.w) aliyetuumba. Sisi binadamu tunajifunza kupitia njia mbalimbali lakini katu hatuifikii mwisho wake.

Mambo mengine yote tunayofuatilia hapa duniani yana kikomo chake.
Matokeo ya walioteuliwa ya MUM yalipotoka nilijenga matumaini madogo ya kuchaguliwa UCEZ, Ndivyo nilivyomueleza rafiki yangu wa Arusha alipotaka kujua maoni yangu baada ya sote wawili kutoona majina yetu kwenye orodha ile.

Matumaini madogo yalitokana na picha ya shaka ya utendaji wa T.C.U niliyoanza kuipata. Hata hivyo kwa utaalamu wa matumizi ya kompyuta nilifikiri kule T.C.U hata kama mtu atachaguliwa na walimu wa vyuo tofaudti alivyoomba, wao wangemuona kwa kufuata programu ya utambuzi wa orodha kulingana na taarifa za muombaji.

Kwa hali hiyo wa T.C.U wangembainisha muombaji huyo kwenye sehemu moja tu. Kuwepo kwa T.C.U. Kwa malengo ya namna hii niliona ni moja ya nia nzuri za kuanzishwa kwake, kuweka bajeti zake na kuondosha dosari za uchaguzi za vyuo vikuu.

Gazeti la Annuur la Ijumaa Agosti 4 likatoa orodha ya majina ya waliochaguliwa Chuo kikuu cha Chukwana (UCEZ), jina langu halikuwemo.

Wakati naendelea kurudia majina kwa fikra kuwa sikuwa nimeangalia vyema kwenye upitiaji wa mwanzo wa haraka haraka, nikapata ujumbe kutoka kwa rafiki yangu akitaka kujua jee nimechaguliwa?

Nikatulia na kuangalia kila Saidi, Mohammed na Masoud walioko kwenye vitengo tofauti, bado kila nilivyowapanga nikakuta sio mimi. Baadae nikamuandikia "Inna lilah wa Inna Ihaih raajiuun. Nako pia sikuchaguliwa.

Morogoro walichagua mia mbili (200) na Chukwani 272; mia mbili na sabini na mbili tu. Naamini ni asilimia ndogo ya walioomba na kuwa na sifa za kuendelea na masomo. Katika majibu yao hakukuwa na kuombwa radhi tulioachwa wala sababu. Pia hakukuwa na maelekezo mengine ya kutuliwaza. Kwa ujumla ni majibu ya kijeuri na kutudharau sote waliotuwacha. Pengine si wao ni jueuri za T.C.U ambazo hata majibu kwa watahiniwa ni kwa kufuata mfumo wa kimataifa.

MBIO ZA VIJITI NA WAPUMBAVU

Ingukuwa ni mbio za vijiti, kwamba anayefikisha mwanzo ndiye mshindi, basi kwa mbio hizi mimi ningelikuwa miongoni wa washindi.
Upande mwengine, ingelikuwa kuchaguliwa kujiunga na vyuo vikuu ni kwa kujulikana na wahusika wa usajili, nako pia kungenisaidia sana. Profesa Issa Kaboko na ustadh Ismail wa MUM walikuwa wakinikaribisha binafsi. Kule Chukwani nako, ustadh Khamisi na wenzake, pamoja na miaka mitano kupita bado walinikumbuka vyema na kunielekeza kwa vizuri.

Msemo mmoja wa kiarabu unasema uwendawazimu una ncha nyingi, hata kuwa na akili nyingi pia ni miongoni mwao.

Yuko "mkichaa" mmoja hupendelea kufika kwenye biashara yetu kwa siku hata mara saba. Kuna vitu viwili tu anavyotaka kwetu, kwanza ni kujua kwenye boksi lolote atakalolikuta mbele yake kumewekwa nini. Chochote atakachoambiwa kimo huridhika na kuondoka. Pili hutaka kujua atapewa shilingi hamsini?.Akiambiwa hakuna au aje baadae huondoka bila tabu. Anaporudi madai ni hayo hayo na chchote anachojibiwa hutosheka na kuondoka kwa usalama. Tumemzoea miaka mingi.

Mwengine alikuwa na iblisi wa kutafuta na kung'oa jani fulani tu pembezoni mwa barabara. Vijana kwa wazee walipoona jani hilo limeng'olewa pembezoni mwa barabara walijua mkichaa fulani amepita hapo ndani ya jiji la Tanga. Mwishowe aligongwa akafa.

Kwa jinsi nilivyofika chuoni Morogoro na Chukwani watu kama Mariamu wa chumba cha mapokezi na baadhi ya walimu lazima waliujua uwendawazimu wangu wa kupenda kusoma. Jibu lolote walilonipatia nilitosheka na sikuvunjika moyo kurudi tena kuulizia. Kila mara waliona majani yangu kwenye meza zao.

Inaonekana ugonjwa wangu huo haukupata dawa sehemu hizo. Sehemu na njia nyengine za kusoma zipo. Hata hivyo kwa kukosa ushindani na mpangilio nyingi ya hizo zinatumia muda mrefu, muda ambao unakosekana.

SALAMU KWA WASOMI.

Katika Qu'an 7:46 na 10:10 kuna maelezo kuhusu salamu kwa waislamu. Kwa kuzingatia hivyo na mimi nawatolea salamu wasomi wetu wa Tanzania, hasa wasomi wa kiislamu. Salamu zangu hizi zinahusu mambo ambayo kwa usomi wangu ningependa niyafanye. Kwa yale ambayo sio kwenye fani yangu, basi wasomi wenzangu niwahamasishe wayafanye kwa faida zetu sote.

Kukutana kwetu naamini kutakuwa rahisi kupitia maandishi tu. Kwenye vyumba vya madarasa na makongamano haitokuwa njia nyepesi tena kwa upande wangu.

<u>KUSAWAZISHA MILINGANYO MPAKA LINI?</u>

Kwenye somo la kemia kiwango cha "O" msemo wa balance of equation" ni maarufu kwa wanafunzi walio wengi.

Kiwango cha kidato cha tano na sita milinganyo hiyo inakuwa ya mazonge zaidi yanayohitaji akili kali kuisawazisha. Ukiingia kwenye kemia kaboni- *organic chemistry;* milinganyo inakuwa mikubwa na migumu zaidi kuisawazisha. Inakaa kimpangilio wa umbile la sega la asali ya nyuki.

Nemewahi kufungua vitabu vya somo hili ngazi za vyuo vikuu nikakuta vitu hivi katika miundo migumu iliyojaziwa vitu vyengine vya kuzingatiwa wakati wa kusawazisha. Milinganyo – *equations,* inapatikana hata kwenye masomo ya Biolojia na fizikia kwa kiwango fulani. Ningependa niikariri angalau miwili ya kemia kaboni, lakini si rahisi kuandikika hapa.

Wale wanaofaulu vyema elimu hii kwenye nchi za Ulaya na Marekani, ndio wanaofanya tafiti zaidi, na wao wenyewe kutumika kwenye viwanda vya kuzalisha nguvu za nyuklia kwa matumizi ya kijeshi na kiraia.

Huku kwetu, waliosoma vitu hivyo na kufaulu vyema, twaweza kusema karibu hawana tofauti yoyote na wale waliokuwa hawakusoma kabisa, kwa jinsi ambavyo elimu zao hazionekani matumizi yake.

Wasomi wetu wanaweza kujitetea kwa kuleta visingizio vingi juu ya sababu ya Tanzania mpaka sasa kutokuwa na mtambo wa kuzalisha nguvu za nyuklia kwa matumizi ya kiraia.

Moja ya sababu inaweza kuwa ni uchanga wa nchi yetu na uchumi wake, na kwamba kitu kama hicho ni cha gharama kubwa kukianzisha.
Pamoja ha hivyo tatizo kubwa laweza kuwa ni sera za kiinchi. Kwa sababu haioneshi kuwa tunaposoma elimu hizi tuna malengo ya zaidi, mbali na kufaulu vyema mitihani, kujipatia vyeti vyenye A- chanya na B zake.

Wengi wa wasomi wetu wanaofaulu vyuoni ndio hawa hawa wanaoingia kwenye bunge. Hawana ushujaa wa kisomi kujadili kuwa na kiwanda kama hicho ambacho Marakeani na Ulaya hawapendi wengine wawe navyo.

Siku moja nilishuhudia ugomvi baina ya watu wawili kwenye foleni ya kuingia kwanye kivuko – feri , mwishoni na mabishano yao, yule aliyevalia suti nzuri akamwambia kum-beza mwenzake aliyevalia nguo chakavu na malapa mguuni "mtu mwenyewe hata kisomo huna wewe, nenda".

Bila kuwa na ushahidi wa kitu cha kisomi cha kuwafaa watu, ni afadhali kukaa kimya. Kwa sababu ukitakiwa kuonesha usomi wako itakuwa tabu. Utaishia kuonesha fotokopi za cheti chako tu.
Binafsi kwa kujua upana wa elimu, najihisi yale niyajuwayo kama nimehudhuria semina tu.

VISHIMO KWENYE ULIMWENGU PEPE.
Ulimwengu pepe- electronics, una mambo mengi yasiyofikia mwisho kuyajua kama zilivyo elimu nyengine zote za Allah (s.w). Yale niyajuwayo mimi pia si kidogo.

Ili tusiwawache wasomaji wengine njiani nitataja yaliyo mepesi tu, yaliyoganda juu ya akili yangu, ili na wao wasiwe gizani moja kwa moja kuhusu ulimwengu pepe.

Takriban elementi zote zilizokwishagunduliwa ikiwemo Tanzanite inayopatikana Tanzania pekee mpaka sasa, zimeundika na atomi nyingi.

Kila atomi ya elementi ina kiini na gamba. Kwenye kiini kunakaa protoni na mara nyengine na nutroni. Kwenye gamba au magamba (shells) huwa zinakaa electroni kwa idadi tofauti kulingana na tabia za hiyo elementi.

Electroni ambazo huwa zinaelea kwenye masafa maalum kutoka kiini – orbits, huwa zinaweza kutibuliwa kwenye makazi yake kwa mbinu tofauti. Hilo linapotokea huwa kunatokea vituko vya namna nyingi. Vivyo hivyo ikiwa mtu atajaribu kubadili muundiko wa kiini cha element – nucleus, Hapa ndipo zinapoanza nguvu za ajabu za nyuklia za madini ya Uranium.
Moja ya namna ya kuzitibua electroni kwenye makazi yake ni kwa kuzipasha moto atomi za elementi hizo. Hapo electroni huwa zinapata nguvu za ziada na kuruka kutoka njia mzingo – orbit, yake ilipokuwa ikielea kwenda utando mwengine juu yake.

Nguvu hizo zinapopungua, electroni, zenyewe hurudi kwenye makazi yake ilipokuwa awali. Kwa kufanya hivyo zinasababisha mawimbi fulani ambayo ni maalumu kwa kila atomi za elementi.

Mawimbi hayo yakiangaliwa kitaalamu yanaitambulisha elementi moja fulani kutoka elementi nyengine. Kwa heshima ya wagunduzi wake safu hizi – series, zimepewa majina ya "Balmer's series" na "Paschen seris". Safu za Hydrogen ni tofauti na safu za Oxygen na kadhalika.

Majaribio haya yalianza kwenye maabara za kawaida, lakini kwa kutumia vifaa maalum vinawezesha kusoma elementi zilizoko masafa ya mbali ya anga za juu ambako binadamu wala hana uwezo wa kufika.

Waya mrefu wa element hasa metali umejaa mabilioni ya atomi zenye mabilioni ya elektroni. Kwa vile zimeshikamana katika urefu wake wote, mtetemo kwa kasi ya ajabu mpaka ncha ya pili. Mtetemo ncha ya mwanzo unaanza kwa kujenga nguvu inayoitwa volti.

Mtetemo wa elektroni kwenye orbit za atomi za elementi hasa za kundi la metali ndiko kunakosababisha mwendo wa nguvu ya umeme.

Hata hivyo umeme si lazima uwe wa mwendo wa mtetemo wa elekroni tu, hata protoni na nutroni pia zinafaa.

Katika haja mahasusi za ulimwengu pepe umeme unatakiwa uwe wa mwendo wa pole, na usimame pale tunapotaka bila kuathiri mwendo wa wenzake ndani ya kifaa pepe fulani mfano kompyuta na redio. Hili linawezekana kwa kutumia madini ya kundi la "Semi Conductors" yenye elementi kama siliconi na Germanium.

Umeme kwenye Silicon ni umeme uliotiwa shemere au ujamu unapelekwa kasi, unapunguzwa mwendo na ikihitajika unasimamishwa kabisa. Vidude vidogo vidogo vilivyotengenezwa kwa Siliconi vinaunganishwa kinamna fulani. Umeme unapoanzishwa upande maalum, elektroni zinapenya kwenda upande wa pili, kutengeneza umeme mwengine utakaotumika sehemu maalum, unaofikia kasi hata sawa na ule wa mtetemo. Huku elektroni zilizoondoka tuna chukulia zimewacha vishimo, vyengine. Vishimo vya elektroni (e) hujazwa na vishimo vya protoni (p). Vyenyewe vipo na athari ya mabadiliko yake yanajulikana lakini havionekani kwa macho.

Mwendo huo wa umeme kwa kujaza vishimo una tengeneza vidayodi ambavyo ni nyenzo muhimu katika kubuni na kutengeneza vifaa mbalimbali vya ulimwengu pepe. Kwa ujumla mwendo wa kasi wa umeme, mwendo wa pole na mchanganyiko wa vitu vidogo vidogo vyengine visivyokamatika vyema mkononi ndiko kunakoleta ulimwengu pepe.

Baadhi ya vifaa au sehemu ya vifaa hivyo huwa havitumii umeme kama unavyozalishwa na mitambo ya umeme (a.c). Vyenyewe hutumia umeme wa (d.c). namna nyengine ya kuuchuja umeme kutoka (a.c) kuwa (d.c) ni kwa kufunika kibati kidogo ndani eneo dogo lisilokuwa na hewa. Vaccuum na kuunganisha waya upande wa pili utakakopita umeme wa (d.c). upande huo wa pili unaitwa Anodi.

Kwa vile anodi ni ya metali aina nzuri zaidi iliyochaguliwa, na metali ina atomi zenye elektroni, nutroni na protoni, kazi inayokusudiwa huwa ni rahisi kufanyika. Umeme uliounganishwa na kibati electrode unapowashwa elektroni hufumuka kwenye kibati na kuelea kwenye vacuuum. Anodi mwanzo huzifyonza elektroni kwa vile inakuwa na protoni nyingine kutengenza umeme wake. Baada ya muda mfupi huzidiwa nguvu na kuziwacha.

Kutokana na mabadiliko ya mwendo wa umeme kwenye elektrodi, punde Anodi hupata njaa tena ya elektroni na kuzimeza tena kutoka vacuum, kutengeneza umeme wake. Ni wazi umeme wake utakuwa ni wa kukatika katika. Huo ni mwanzo tu wa mchujo tuwache hapo. Dayodi zaidi ya kuchuja pia huwa ni vali ya umeme. Tunayoyajadili yanatokea kwa kasi ya ajabu hata jicho halina uwezo wa kuona shughuli hiyo.

Hayo niliyoyataja hapo juu si chochote kuliko yanavyojulikana na wasomi wetu wa masomo ya sayansi hasa wa tawi la ulimwengu pepe ndani ya somo kuu la fizikia. Kujivunia kufaulu kwao tu katika daraja za juu na aina ya alama msomi husika aliyopata.

Wengi wetu tunakuwa na uhodari tu wa kubonyeza bonyeza vifungo vya vidude vilivyotengenezwa wakati mwengine na watoto tu wa nchi za wenzetu. Wakati mwengine tunashindwa na hata watundu waliomaliza darasa la saba na kukosa fursa za kuendelea na masomo.

Tatizo pengine ni madhumini ya mfumo wetu wa elimu na sera za kiinchi. Mpaka sasa sijasikia Tanzania kuwa na kiwanda chochote cha angalau kuunganisha tu vitransistor na vidayodi kutengenezaa vidude rahisi vya kilimwengu pepe.

Ambapo hata tungeunganisha vikokotoo vya kuzia sokoni, basi soko lake la ndani lingetosha kupata faida ya kiwanda kujiendesha chenyewe bila msaada wa Marekana na A.U. na kama bidhaa zingeongezeka kuhitaji soko la nje, basi wenzetu, majirani zetu warundi, wakongo na waganda wangekuwa wateja wetu wazuri.

Lakini iwapo usomi Tanzania unapimwa kwa vyeti, na ndio unaozingatiwa kwenye ajira hata kwenye ofisi ya raisi ambako hakuna kiwanda pepe, basi waislamu nasi hatuna budi kwenda kulingana na hali, huku tukijiwekea malengo ya mbali kielimu kulingana na dini yetu.

KIWANGO CHA ELIMU KIMEKUWA

.Waislamu tusidumazwe na ukiritimba wa elimu wa kikafiri.

Waziri wa elimu profesa Jumanne Maghembe kwenye Gazeti la Mwananchi la 20/10/2008 alikiri kuvuja kwa mitihani ya kidato cha nne ya mwaka 2008.Alieleza hayo wakati akihutubia mahafali ya kumaliza kidato cha 4 kwenye shule ya Kighare-Usangi.Hata hivyo

yeye alikiri kuvuja kwa mtihani wa somo la hisabati tu,althibitisha kuvuja huko kwa karatasi ya mtihani aliyopelekewa usiku tarehe 5/10/2008 na wakalazimika kuifuta.

Alikanusha kuvuja kwa mitihani mengine na akasema mengine iliyotajwa kuvujwa ilikuwa ni miradi ya matapeli tu ambao walitayarisha mitihani yao na kuiuza kwa sh 300,000.Kwa mradi huo alisema matapeli waliweza kuvuna mpka sh 18,000,000.Vile vile aliwalaumu wazazi waliowapa fedha watoto wao ili wakachangiane kununua mitihani hiyo.

Mwaka 1998 mitihani yote ya baraza la mitihani ilibidi ifutwe kutokana na tatizo hilo la wizi na kuvuja.Waziri wa elimu amejibu kisiasa kwa kuhofia usumbufu kwa upande wake na kwa taifa pindi angekiri kuwa mitihani ilivuja sana.Kwenye gazeti la Majira la 12/10/2008 katibu mkuu wa baraza la mitihani (NECTA) bi Dkt Joyce Ndalichako aliripotiwa akikiri kuvuja kwa mtihani mwengine wa Civics.

Polisi mikoa mbali mbali waliwakamata wanafunzi wa shule kadhaa wakiwa na majibu ya mitihani na wengine wakijigamba kuwa majibu hayo ni sawa na mitihani waliyoifanya.Walipohojiwa walieleza kuwa huwa wanapeana taarifa na majibu kwa kupitia simu za mikononi.Gazeti la Nipashe liliripoti watu wanaodhaniwa kuwa ni majambazi wakiwa na silaha waliovunja shule ya sekondari ya Ngateua wilayani Arumeru na kuiba mitihani.

Wizi na udanganyifu katika mitihani na matokeo ni tatizo la kila nchi.Polisi nchini Uganda waliwakamata watu wakiwa na mitihani ya kidato cha nne ambayo ilianza takriban siku moja na ile ya Tanzania iliyoanza tarehe 6/10/2008.Tarehe 8.11.2008 nilisoma kwenye mtandao wa internet habari ya waziri wa Iran ambaye alikabiliwa na tuhuma za kughushi vyeti vya chuo kikuu.

Kuna mengi ya kujadili kuhusiana na udanganyifu na wizi wa mitihani na upatikanaji wa vyeti bandia,lakini muhimu ni kukazia ile nukta kwamba kwa waislamu si suna kupima usomi wa watu kwa kuangalia vyeti na daraja zao.

Mwalimu wetu Bi Dr.Victoria Muwonge kutoka Islamic University of Uganda (I U I U) alifika chuoni MUM kututembelea na akapata kuzungumza na wanafunzi kwa dakika 30.Sisi tunaosomea chini ya miti tulilmsikia kupitia gazeti la Horizon,toleo na.005 la May 30-June 5,2007 ukursa wa 6 kama ilivyoripotiwa na Abdul Wakil S.Saiboko.

Katika hotuba yake alisema "*We have to learn many things and we have to obtain that knowledge from many sources.Education is not necessarily what you write down in an examination*".Tafsiri nyepesi ni kuwa alikusudia tutafute elilmu kutoka sehemu mbali mbali na kwamba elimu si lazima iwe ni ile mtu anayoifanyia mtihani.Baada ya hapo akahimiza sana elimu ionekane kwenye vitendo.

Hapo nilimuona kaenda sambamba na maana ya elimu,hata hivyo mwisho alijichanganya na kunichanganya na mimi ,pale alipoupongeza uamuzi wa MUM kutokuchua na kusomesha wanafunzi wengi.ili kulinda ubora wa elimu na hadhi ya chuo.

Huu ni ushahidi jinsi wasomi walivyohadaika na maana ya elimu kiasi kwamba hata waislamu wamefuata mkumbo huo.Ili watu wafikie viwango vya kukubalika katika vyuo hivi hutokea uovu wa kila aina na udanganyifu.Utawaona waislamu wake kwa waume wakipenya huku na huku bila haya ili kujaza fomu za kuwawezesha kupata mikopo ya fedha na matokeo ya kuwafanya wastahili kuchaguliwa kusoma kwenye vyuo vyenye ukiritimba mwingi.

Mmoja ya wanafunzi waliofukuzwa kutoka Pakistan na kibaraka Pervez Musharaf kutekeleza sera za Marekani, siku moja tulikutana akawa akisoma kwenye gazeti tangazo la maombi ya kujiunga na chuo kikuu kimoja.Akasita alipofika kipengele cha umri wa

muombaji.Akaniambia “sheikh! angalia mambo haya ati umri wa muombaji usizidi miaka 30.).Akauliza haya yametokea wapi tena,akataja hadithi za Mtume (s.a.w) ambazo hazina vipengele vya umri na daraja.

Katika Qur’an elimu imepewa kipaumbele cha kuwa iwe ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.Ndivyo aya za mwanzo kushuka katika surat Alaq zilivyobainisha.(96:1-5).Nabii Adam (A.S) alifundishwa elimu zote na Allah (s.w) (Qur: 31-32).

Nabii Daud (A.S) alikuwa ni fundi wa kutengeneza mavazi ya kivita.(Qur:21:80).Katika ulimwengu wa sasa nabii Daud anaweza kuwakilisha wahandisi na viwanda vikubwa vya kutengeneza zana za kivita kwa ajili ya kuilinda dini ya Allah (s.w).

Uadiliflu ni sifa ya Mwenyezi Mungu,kwa uadilifu wake huo amejaalia njia za kupatia elimu ziwe nyepesi na za wazi kwa kila mwanadamu nazo ni kama vile akili,midomo na ulimi wake,masikio na macho.Mfumo wa elimu sahihi unatambua wenye elimu na wasio na elimu (Qur Azzumar:9), lakini haujataja vyeti wala daraja ya kujua.Kwa kila mwenye elimu basi ana sehemu tu ya elimu na wako wenye kujua zaidi kuliko yeye.

Kwa kutumia akili na nyenzo za kujielimisha nabii Musa (A.S) aliandamana na nabii Al Khidhri ili ajielimishe zaidi (Qur 18:66).Hatua hii ni kutekeleza agizo la Mwenyezi Mungu katika kujielimisha yaani kuwauliza wenye kujua zaidi yako; Qur (16:43).Mtume (s.a.w) kasema Elimu ni hazina na ufunguo wake ni suali (kuuliza).

Waislamu tumehimizwa katika hadithi ya Mtume (s.a.w) tuwe wenye elimu au wenye kutafuta elimu au wasikilizaji wa elimu,lakini tusiwe wajinga.Hata kujua aya moja na kuwa tayari kuifanyia kazi na kuifikisha kwa wengine nayo pia ni elimu (hadithi na. 182:mishkaatul maswaabih)

Katika hadithi nambari 1,821 katika Muwatta ya imam Malik, mja mwema Luqman alipokuwa akimuusia mwanawe alimwambia Ewe mwanangu kaa na wenye elimu na uwaheshimu kwani kwa hakika Mwenyezi Mungu huzipa uhai nyoyo kwa nuru ya elimu kama vile anavyoipa uhai ardhi kwa mvua kutoka mawinguni. Elimu imetajwa kuwa ni faradhi kwa kila muislamu.Kote huku hakuna umri,cheti wala daraja.

Vitendo ni kipimo bora cha kuonesha elimu ya mtu na si cheti.Akina Osama na vijana wenzake walitaka waruhusiwe kwenda vitani.Kwa umri wao walikataliwa.Ilibidi wapimwe uwezo wao kwa vitendo vyao vya kumududu kutumia silaha.

Si vibaya kwa mwenye kujiona ana elimu fulani itakayosaidia ibada za waumini kupendekeza kuitumia.Nabii Yussuf (a.s) alipendekeza apewe kazi ya kutunza hazina kwa kujiamini na elimu yake.Majini kwa nabii Suleiman walipendekeza kutumia elimu zao ili kukileta kiti cha malkia Bilqis.

Kuruhusu vipaji vya elimu na kuwasikiliza watu na rai zao ni suna katika uislamu.,hasa sehemu yenye mzozo.Nabii Muhammad (s.a.w) alimsikiliza sahaba wake Suleiman Al farsy wakati wa vita vya handak na rai yake ikatokea kuwa ngome na nusra kwa waislamu.

Elimu kwa ajili ya Allah (s.w) kwa vile ina malengo ya akhera zaidi hata ukiwa mzee kiasi gani bado ni haki yako mja kujifunza,inawezekana na ina faida.Bibi yangu mmoja mwaka huu shawwaal 1429-H ana miaka zaidi ya 110.Katika miaka ya hivi karibuni amekuwa akijibidiisha sana kusoma Qur’an na kutekeleza ibada nyingi.Karibuni hivi ameuza baadhi ya mali zake na fedha za mauzo hayo kaziingiza kwenye mambo kadhaa ya kheri.Umuhimu wa kufanya hivi bila shaka umetokana na elimu ambayo amejiongezea karibuni.

Hayo tuliyoyaeleza ni baadhi tu ya tunayoyajua kuhusu elimu.Hata hivyo maana ya elimu na matumizi ya elimu kwa kipimo cha matendo ya wanaoitwa wasomi inadhihirika bado

haijaeleweka vyema.Ubaya ni kuwa kutoeleweka kupo hata kwa waislamu ambao wana muongozo sahihi wa elimu.

Kutengwa kwa waislamu ambao hawakupitia shule zilizoanzishwa na makanisa kwa madai kuwa hawakusoma kulianza kusemwa na wakristo.Miaka ya hivi karibuni mijadala mingi inayoibuka kuhusu waislamu kutoajiriwa kulingana na wingi wao katika nafasi muhimu za kiserikali na katika maofisi ya umma,imekuwa ikififilizwa kwa madai kwamba waislamu hawakusoma.Waislamu wana ushahidi wa kutosha kwamba ikiwa kusoma ni kwa kupitia shule basi hawajawahi kudharau elimu bali wamebagulilwa tangu wakati wa ukoloni mpaka katika serikali za baada ya uhuru.

Upungufu katika kujitetea huku ni kuwa waislamu hawatetei maana ya elimu.Kwa kusahau huku,huwa kama kwamba wanahalalisha kubaguliwa huko katika ajira,kwa sababu ni kweli kwa ubaguzi wa mwanzo waislamu waliofikia viwango vya elimu vya kiserikali ni wachache kuliko wakristo.Lakini jee kuelimika ni kwa kupitia shule zinazotambulika na serikali na kufanya mitihani kutoka wizara ya elimu tu?.

Kipande kutoka kitabu cha *Islam and politics in Tanzania* cha Mohammed Said kinathibitisha kuwa waislamu walikuwa ni wasomi wa mwanzo Tanzania,na kwamba ndio wafanyakazi wa mwanzo serikalini.Uandishi wao ulikuwa kwa hati rasmi za Qur'an yaani kiarabu. Hili linadhihirika kwa wajerumani kumkuta chief Kimweri na wanawe kuwa ndio wajuzi pekee waliowakuta ,walioweza kuandika na kuhesabu.

When colonialists and missionaries set foot in the East African coast then known as Zanj their main aim was to wipe out Islam. Muslims in the East African coast had their first glimpse of what Christianity was all about in 1498 with the arrival of the Portuguese. In 1567 the Augustinian order was established in the East African coast to counter the influence of Islam so that Christianity becomes the religion of the whole world. Christianity extended its influence further when Cardinal Lavigirie founded The White Fathers, the Catholic institution whose purpose was and still is to confront Islam.(1) About the same time period Church Missionary Society (CMS) imposed upon itself the duty to deliver the world from Islam, ignorance and darkness.(2) The White Fathers are in Tanzania and are still involved in the work which brought them to the country more than a hundred years ago.

When the Germans first arrived in Tanganyika they found Muslim already literate, they could read, write and count. The missionary Ludwig Krapf when he appeared at the court of Chief Kimweri of the Sambaa in 1848 he found him and his children literate. They could read and write with ease. (3) The alphabet in use was the Arabic script. Being educated Muslims were employed by the German colonial government as teachers, interpreters and administrators. The institution responsible for all this excellence and achievement was the madras. Missionaries and colonialists were envious of the level of educational advancement achieved by Muslims and therefore initiated plans to subvert its progress

Ukweli huu umesahaulika na masheikh zetu na wasomi waislamu waliosoma katika shule za kiserikali kutokana na mashinikizo ya kejeli kwa waislamu.Matokeo yake masheikh wengi wamekubali kuwa hawakusoma.Wanapoingia maofisini kutaka huduma huingia kwa unyonge sana wakati mwengine kwa udhalili hata kuvua mavazi ya utamaduni wa kiislamu au hata kuhofu kutoa salamu ya kiislamu.Mwezi oktoba 2008 nilifika benki ya CRDB tawi

la Tanga nikakutana na sheikh fulani ninayemfahamu mavazi yake kuwa ni kanzu na kofia.Siku hiyo nililmkuta akiwa na suti,sijui alikwenda kufuata huduma gani siku hiyo.

Masheikh hawa hawadai chochote kutoka serikalini na hawaombi nafasi za kufanya kazi katika taasisi za serikali na umma.Hawashangai kuona mabaraza ya miji na mipango miji yametawaliwa na wakristo watupu ambao huzigawa ardhi za mababu zao waislamu kwa watu wanaowataka mwanzo kabla watu wengine na wenyeji kupewa.Kwenye ofisi za mipango miji Tanga mimi binafsi na mdogo wangu tumepeleka maombi kwa fomu na malipo,hata hivyo eneo tuliloombea limegawiwa kwa waombaji wengine bila sisi kuaarifiwa.

Masheikh hawajishughulishi na siasa kuwawezesha kuingia bungeni na kuchangia mambo ambayo hupitishwa na kuwa sera za kuendesha nchi.Wamejitenga na hata kuzungumzia mambo muhimu ya kiadui yanayotendeka katika jamii angalau tu wanapokuwa misikitini mwao.

Mwezi huo;Oktoba 2008 wakati kampeni za uchaguzi wa rais wa Marekani kati ya Barack Obama na John McCain zinakaribia ukikungoni na kipindi cha urais wa adui mkubwa wa uislam George Bush kinakaribia kwisha.Kipindi hiki kilikumbwa na hofu kubwa ya uchumi wa dunia.Mabenki mengi kote Ulaya na Marekani yamekumbwa na wasi wasi mkubwa.Hatua zote zilizofanywa kurekebisha hali hakujawa na matumaini.Makala mbali mbali za uchambuzi zimeandikwa kuielezea hali hii,miiongoni mwao ni *Is this the end of American Imperialism*?.

Sheikh Hassan Ahmed kutoka Mombasa ametoa changamoto kuwa maprofesa wa ulimwengu mzima wa masuala ya uchumi wanaelekea kushindwa kutoa jawabu,lakini nabii Yussuf (a.s) peke yake aliweza kuliokoa taifa lake kutokana na janga la njaa. Hivyo si kweli kuwa masheikh hawana elimu za kulitumikia taifa.Sheikh Hassan alifika kututembelea chuoni MUM,sisi tumemsikia kupitia redio Imani.

Ambao hawawaamini masheikh kushika nafasi za uongozi katika serikali si wakristo peke yao,mara nyingi tumewasikia wasomi wenye digrii za vyuoni walizozipata hapa nchini au nje wakiwabeza masheikh hawa.Vipimo vyao vya elimu ni sawa na vile vya kikafiri.Umuhimu wa kuwatumia masheikh hawa ni pale wanapofikwa na matatizo tu.

Mwezi Juni 2008,magazeti ya kiislamu nchini yalijitahidi kuwaelimisha waislamu kuhusu mpango wa kamisheni ya vyuo vikuu Tanzania (T.C.U) wa kutaka kuchukua mamlaka ya kudahili wanafunzi wanaotaka kujiunga na vyuo vya elimu ya juu.Gazeti la Alhuda la Jamadul Aakhar 1429;Ijumaa Juni 13-18;2008 liliandika likimnakili skh Kilaghai:*Ni lazima kila mmoja wetu ashiriki kikamilifu katika jambo hili ,kuanzia ngazi ya msikiti.Maimamu wa misikiti yote walizungumze suala hili katika khutba na mawaidha misikitini*.

Pamoja na kwamba masheikh wenyewe wengi,wenye misikiti hiyo wamelala na hawajishughulishi na kufuatilia njama kama hizo,lakini na hao wasomi wenyewe wanaotaka msaada huo hawaonekani kuwa wakweli katika kutambua umuhimu wa

masheikh hawa na taasisi za misikiti.Sijawahi kusikia juhudi yoyote ya kutaka mfumo wa elimu wa kiislamu utambuliwe rasmi.

Katika hali kama hii ni kama kuwaburuza masheikh watumikie jambo wasilolielewa na ambalo manufaa yake kwao ni madogo.Kwa kukosa uelewa wa jambo kama hili mara nyingi maombi kama haya kwa masheikh hukosa watekelezaji,isipokuwa wachache.

Msomi mwenye shahada mbili au tatu za lugha ya kiengereza,kwa kweli ni msomi na mtu muhimu katika fani yake.Lakini kwa hakika elimu yake si kigezo cha elimu yote.Kama yeye anavyoweza kutaja mambo yanayoweza kumtia kizunguzungu sheikh.Msomi huyu hana tofauti na umuhimu wa sheikh aliyebobea kwenye nahau na balagha,sheikh akichambua mnyambuliko wa maneno katika tungo hatosikia neno na lazima naye atakipata kizunguzungu.

Katika siku za karibuni za hizi enzi zetu,ujuzi wa kompyuta imeonekana ni moja ya dalili za usomi,wakati mwingi mafunzo ya kompyuta hutumika kuwavutia wazazi kupeleka watoto wao kwenye shule zisizo na maadili wala malezi mazuri.Lakini kompyuta si kwamba haisomeki kwenye madrasa au ni lazima iwe kwa lugha ya kiiengereza.

Aliyesomea uhandisi wa kompyuta au udaktari bingwa wa masulala mbali mbali ya kiafya, iwe hapa nchini au Ulaya ni msomi muhimu sana na kweli ana elimu.Lakini elimu yake si kigezo cha elimu yote na kuwa sababu ya kujikweza na kuwanyongesha wasio na elimu kama ya kwake.Vivyo hivyo yule anayeendesha mitambo ya kuzalisha na kugawa umeme ni msomi muhimu sana lakini haingii akilini kuwa elimu yake hiyo imtie kiburi cha kuwakejeli masheikh na maustadh kwamba hawakusoma.

Mwenye ujuzi wa kuezeka bati hata kama hakwenda shule yoyote naye ni msomi anayepaswa kuthaminiwa kwa elimu yake hii.Katika hali ya kibinadamu na isiyo rasmi huwa anathaminika kwani wasomi wa kila aina humtegemea yeye kwa kazi zao za aina hiyo.

Athari za kuthamini elimu kwa vyeti inawapelekea masheikh kuwathamini watu ambao wao walitakiwa kuwadharau na kuwakemea kwa kufru zao.Mtu ambaye ana digrii mfano ya mambo ya viumbe pamoja na evolusheni,anayejua vyema hatua za mtu kugeuka kutoka kuwa nyani.Huyu si msomi bali ni mjinga tu ambaye wala si wa kuthaminiwa.Inasikitisha masheikh huwanynyekea hawa kama wasomi.

Mara nyingi sana huwa tunaoneshwa kwenye maruninga watu waliovaa vibaya vibaya wakifanya mambo ya ovyo ovyo na huku wakichambuliwa sifa za usomi wao.Baadhi ya wanafunzi wa vyuo vikuu kwa kweli huwa wanatenda mambo ya kijinga na kijuha kuliko watu wa shamba yoyote.

“Panya Buku Wahitimu chuo kikuu”

Matokeo ya kuthamini elimu ya vyeti sasa imefikia hata wanyama na wadudu kupewa hadhi ya ubora kuliko binadamu.Katika gazeti la Mwananchi la tarehe 12 Juni 2008,ukurasa wa 3 kulikuwa na habari iliyosema ‘Panya buku wahitimu chuo kikuu”

18 wapelekwa kufanya kazi ya kunusa mabomu Msumbiji

Panya wahitimu Chuo Kikuu cha SUA

Mmojawapo wa panya wanaotumika kunusa mabomu ya kutegwa a
cha Kilimo (SUA) cha APOPO.

Na Michael Uledi, Dodoma

utaalam huo,"a lisema Dk Mathayo na kuongeza kwamba panya hao hawauzwi.

Naibu Waziri huyo, alisema kuwa pa-

ya mlipuko na hivyo hawasababishi uharibifu mkubwa wa mazao.

"Aidha Wizara inapenda kutoa ufafanuzi kuwa panya hao wanafundish wa kuvumbua eneo ambalo lina mabo mu yaliyotegwa ardhini kwa kunus

Katika habari hiyo ilielezwa kuwa wahitimu hao wa chuo kikuu cha SUA wa fani ya mabomu,ilikuwa waondoke nchini kuelekea Msumbiji kusaidia kutegua mabomu ya tokea wakati wa vita vya wenyewe kwa wenyewe baina ya FRELIMO na RENAMO.Ni kweli kuwa panya hao wana elimu katika fani muhimu ya ustawi wa jamii,lakini si bora na wala si wa kuthaminiwa zaidi kuliko binadamu wengine ambao hawajapitia chuo kikuu.

Kwa ujumla usomi wa vyeti umechangia kubaguliwa waislamu katika ajira,kitu ambacho kinadumaza kiimani kwa kuwapa nguvu za kiuchumi wakristo na kuwafukarisha waislamu.Hali hii imepelekea maeneo muhimu katikati ya miji ya kiislamu kuchukuliwa na wakristo waliowezeshwa kiuchumi na mfumo wa ajira wenye kuthamini vyeti.

Zaidi ya kwamba vyeti haviaminiki kwa kukosekana uadililifu kwa watahiniwa na wasimamizi wa mitihani,lakini ukweli ni kuwa elimu mtu aisomayo, nyingi hubaki kwenye madaftari tu na chache huganda akilini.Inayotumika ofisini ni ndogo sana kiasi kwamba kila ambaye si taahira akipewa semina fupi ana uwezo wa kuzimudu kazi za kiofisi.Mfano mtu anaweza kuwa amesoma sana historia ya wanafalasafa na wanasiasa mfano habari za Aristotle au Winston Churchil. Mwengine ni mwanahisabati na hodari sana kusarifu herufi za x, y,i na kadhalika.Lakini ofisini akawa kazi yake ni kuandika sentensi fulani fupi fupi tu kuwajibu wenye shida katika ofisi hiyo.Jee kazi hiyo ndiyo ya kulazimisha kwamba lazima afanye yeye na sisi wengine hatuwezi kuifanya?.

Iko athari nyengine mbaya ya kuthamini elimu ya vyeti,hii ni katika kuupiga vita uislamu bila silaha za moto.Wako ambao wana vyeti vya daraja za juu lakini matendo yao hayaendani na vyeti vyao.Kuwa imamu au mkuu wa taasisi ni aina ya cheti.Yanapotokea masuala muhimu yanayoihusu jamii ya kiislamu na maadui wa uislamu wakawa na maslahi upande wao, hawasiti kupitishia misimamo yao kwa watu hawa wenye vyeti huku wakiwajua matendo yao ni kama ya kwao.Kauli za wasomi hawa hushinikizwa kwa waislamu wote kwa mitindo mbali mbali, hata kama ukweli ni tofauti na hivyo.Ukweli hunyamazishwa kwa kisingizio kuwa wengine hawajui kwa vile hawana vyeti vya kusemea.

Siku za uchaguzi wa kidemokrasia ni msimu wa dhulma na ushenzi wa kila aina.Mbali na kubambikiwa makosa watu kama mimi kwa lengo la kuwatisha wengine,wasomi wa vyeti hutumika kubuni takwimu za kuujenga upande fulani na kuubomoa mwengine.Nakumbuka takwimu za taasisi moja kwa misimu miwili ya uchaguzi zilivyotumika kukiponda chama cha CUF ambacho waislamu kwa kuchanganyikiwa na dhaluma wanazofanyiwa walionesha kukimbilia.Badala yake chama cha CCM kikapambwa kitakwimu kuwa ndicho kizuri pekee.

Katikati ya mwaka huu-2008,waziri mkuu Mizengo Peter Pinda aliropokwa jambo kuhusu muungano wa Tanganyika na Zanzibar,ya kwamba Zanzibar si nchi.Kauli hii ilitibua mambo na kuonekana kuwaunganisha watu wote wa Zanzibar ambao wengi ni waislamu.Baraza la wawakilishi ambalo kwa hila za uchaguzi huonekana kutawaliwa na CCM lilionekana kuwa msimamo mmoja baina yao na CUF.Wengine wanasema alilileta hilo kimtego,lakini naamini Pinda alilijutia kwani umoja wa wazanzibari haupendwi.

Wiki iliyopita ilianza habari kwenye gazeti la mwanachi kuwa” *mji wa kale wagunduliwa chini ya bahari”*.Juzi tarehe 20/12/2008 kwenye gazeti la Mwanachi profesa Chami amerudia ugunduzi wake kuwa amegundua njia ya miguu chini ya bahari baina ya Bagamoyo na Makunduchi iliyotumiwa miaka 3000 kabla ya kuja Kristo.Enzi hizo Makunduchi upande wa Zanzibar na Bagamoyo upande wa Tanganyika watu walikuwa wanakwenda kwa miguu kwa vile ilikuwa ni pande moja la ardhi.

Ikiwa ni ugunduzi wa kikweli sipingani nao,lakini najua kuwa maeneo kama haya baada ya kushindwa na hoja na kuutoa mkataba wa Muungano uliovurugwa wasomi wa vyeti ndiyo maeneo wanayotumika kunyamazisha mambo.Ambao mpaka sasa wameshindwa

kupika hoja ni maaskofu wa Tanzania waliosema hivi karibuni kuwa hoja za kurudishwa mahakama ya kadhi Tanzania na kujiunga na OIC kuyajadili bungeni ni ujinga.

Majibu ya kisomi ya masheikh hawakuyatarajia,walidhani vyeti vyao ni bora na ndio tiketi ya kuwatukana waislamu.Wamejua kuwa vyeti vyao si bora kuliko vya madrasa kwani wimbi la kuzinduka waislamu limezidi matarajio yao.Badala yake wao na serikali inayowaunga mkono wametumia silaha yao maarufu ya kukaa kimya bila kujibu mpaka sasa.

Watu wanaweza kuhoji,sasa jee tutajuwaje msomi ni yupi ?,au tutumie vigezo gani kujua wa kumuweka mbele kwa usomi wake bila kutumia vyeti ?. Qur'an 9:105 inatwambia :

وَقُلِ اعْمَلُوا فَسَيَرَى اللهُ عَمَلَكُمْ وَرَسُولُهُ وَالْمُؤْمِنُونَ وَسَتُرَدُّونَ إِلَى عَالِمِ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ فَيُنَبِّئُكُم

بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُون

Na sema:Tendeni vitendo.Basi Mwenyezi Mungu ataviona vitendo vyenu ,na Mtume wake na waumini, Na mtarudishwa kwa mjuzi wa siri na dhahiri;naye atakwambieni kwa yale mliyokuwa mkiyatenda.

Kwa hivyo cheti hasa ni siku mja atakaporudishwa kwa Mola wake,lakini kwa hapa duniani uzuri wa matendo ya mtu hujulikana na watu wema kwa kupima jinsi mtu anavyotekeleza kwa vigezo vya kitabu na suna.Kwamba kila anayetenda sawa basi tendo lake hubarikiwa na kudumu katika hali ya uzuri.Raisi anayefanya vizuri raia wake ndio watakaopima,na iwapo anavyotenda ni vyema, basi lazima atapendeza hata maadui wakimkatalia.Kinyume cha hivyo hata akipewa vyeti vingapi kupambwa kwa matendo yake kwa wale wenye maslahi naye, basi lazima atachukiza kwa watu, na mwisho wa habari vyeti alivyopewa vitaonekana kuwa ni bandia machoni pa raia na wanaoongozwa naye.

Iwapo ni kujua yupi ni daktari mzuri wa kutibu maradhi yetu,ni kuangalia tu wagonjwa wanamfahamu daktari yupi zaidi.Kila daktari lazima ataanza na majaribio,iwe ni kupasua panya au vyenginevyo, Hayo ndiyo yatakayomtambulisha ubingwa wake.Haisaidii kushinikiza uhodari wa daktari kwa wagonjwa kwa vile tu ana cheti cha udaktari bingwa.

Kwa mtindo huu wa kuthamini usomi kwa mtazamo wa kikafiri, kelele tunazopiga waislamu kuhusu kubaguliwa kielimu huku tukilinganisha idadi ya vyuo vinavyomilikiwa na wakristo dhidi ya vile tunavyomiliki.Kwa sasa kwa Tanzania waislamu tunalalamika kuwa tuna MUM tu.Baadhi ya vyuo vya kikristo tunavyojilinganisha vinafundisha Divinity.Bila kuvipa hadhi vyuo kama vya TAMTA,ZAHRAU,CHANG'OMBE na vyenginevyo vingi, na kupigania vitambulike kama vituo vya elimu, basi pengo baina yetu halitazibika,na daima tutaridhia kuongozwa na watu wajinga kuwaona kuwa ni wasomi.Hivyo wizi kama wa EPA na kashfa kama Richmond hazitakwisha wala kupungua,na tutakuwa na mwisho mbaya akhera,Mwenyezi Mungu atuzindue na atuepushe.

Maelezo haya yote hayana lengo la kupinga elimu,kinyume chake ni kuihimiza elimu na kutoa mbinu na zana za kusomea chini ya mti.Kwamba elimu na kusoma ni jambo lililorahisishwa mno,sisi binadamu kwa malengo ya kidunia,sasa ndio tunaoiwekea vikwazo na kuifanyia biashara elimu.Umuhimu wa elimu na kushindana katika kuitafuta na kujenga vituo kwa ajili hiyo,uko pale pale.Muhimu zaidi kama waislamu tubadili maana ya elimu.

Ni kawaida ya binadamu kupenda kutukuzwa kwa lile alilo nalo.Hata wake wazuri pindi wasipokuwa na maadili kikamilifu,hata wakiwa wake wa masheikh ni tabu kuwaweka ndani moja kwa moja.Lazima siku moja moja atapenda aoneshe uzuri wake aliowashindia wenzake.Kwa maana hiyo maelezo ya kupunguza hadhi ya elimu kwa vyeti yatapata upinzani kwa wenye vyeti hivyo.Hata hivyo wasomi wenye vyeti ambao ni waadilifu watakubaliana na mimi kuwa elimu yoyote iliyotajwa kwenye vyeti vyao ni kama semina tu kutokana na ukubwa wa elimu.Wenyewe lazima wamekutana na watu wadogo wasiopata vyeti ambao wanawashinda kwa tawi Fulani la elimu hiyo hiyo aliyopatia cheti.

Binafsi nathamini sana mipango mizuri ya kutenda mambo na nachukia sana ubabaishaji na udanganyifu.Najua kwamba uvumbuzi na ubunifu si mambo mapya na kuwa ndiyo hadhi na milki ya wazungu kama ambavyo wale wanaowabeza waislamu wakati wetu huu, hujaribu kuifanya hoja.Nina ushahidi wa mipango mizuri ya kivumbuzi ya masheikh wengi wa zamani ambao historia haitaji vyuo walivopatia vyeti.

Ubunifu + Uzoefu = Ufumbufu { U+U=U}

Natambua kuwa watu wanaoitwa masheikh tulionao hivi sasa,wengi wanatia aibu na bila kuongezewa nyenzo na vipengele vya kielimu, wakipewa nafasi serikalini watautukanisha uislamu.Natambua kuwa wengi wao wakikaa ofisini badala ya kutenda kiislamu huwa na tabia wakristo wanayoiita ya Uswahili.

Najua kwamba kwa malengo ya haki, Mwenyezi Mungu (s.w) kawajaalia binadamu kuwa ni wenye vipaji tofauti tofauti vinavyotegemeana.Naelewa kwamba wale wanaosoma na kupata vyeti vya daraja la juu ni dalili ya uwezo mkubwa wa kufikiri kwa akili zao na kwamba ni watu wa kutegemewa iwapo vyeti hivyo vimepatikana kwa uhalali.Hata hivyo siamini kuwa wenye vyeti hivyo ndio wajuzi wa kila jambo.

Mwalimu mwenzetu mmoja alipata nafasi ya kwenda kusoma masomo ya juu ya hesabu na fizikia nchini Marekani.Uwezo wake wa kuyafanya mahesabu magumu ulimfanya afikie jawabu bila kupitia njia zilizowekwa na bila kutumia zana za kukokotolea.Jambo hili liliwaudhi wahadhiri wake,matokeo yake hakufikia mwisho wa masomo ikabidi arudishwe nyumbani.Kwa uwezo wake wa kupasisha wanafunzi wengi, wanafunzi walimpenda sana lakini aliwaudhi na kuwaaibisha sana kila mara alipokuwa akiokotwa kwenye mitaro asubuhi matokeo ya ulevi wa kupindukia usiku usiku.Sasa sijui ni yupi bora zaidi kati yake na yule ambaye hakupitia shule kabisa na mwenye kuishi maisha ya kiuchamungu na kujiheshimu.

Kijana wetu mmoja ambaye tumemlea na kumsomesha kwa tabu,mwaka huu 2009 yuko mwaka wa tatu chuo kikuu cha serikali ya Zanzibar (SUZA).Juzi moja tulipanda meli moja kuvuka bahari.Jinsi alivyovaa kimagharibi nilishindwa hata kumuuliza fani ya masomo asomeayo.Alikuwa amevaa bukta ambayo naamini hupatikana kwenye marundo ya mitumba siku za soko kwa bei nafuu sana.Juu alikuwa amevaa kapelo.Yawezekana mwenyewe anajiona msomi sana lakini nikimlinganisha na wakati wa utoto wake, mimi nilihisi amezidi kuwa mjinga.

Kwa ujumla kutokueleweka kwa maana ya elimu kumedumaza sana maendeleo ya kielimu.Wanafunzi na wazazi wako tayari kutoa pesa nyingi kununua mitihani na matokeo.Kutokana na papara ya kupata matoekeo ya mitihani ya daraja Fulani,wazazi na watoto wao wala hawajali mambo yanayofundishwa ambayo baadhi kwa kweli wala si elimu za maana,bali ni wazimu tu na upotofu.Serikali ilipaswa kila baada ya muda itafiti mada za kufundishwa mashuleni kwa kuwashirikisha wazazi.

Kwa vile elimu hukusudiwa kuwaelekeza watu serikali inakotaka hilo halifanyiki.Matokeo ya kampeni kama hizi za muda mrefu hata wazazi wa kuhoji mada za kufundishwa hawapataikani.Wanachojali wazazi ni mtoto wao kupata “A” au “B” tu hata ikiwa ni somo la kukariri katiba za vyama au masuala mengine ya kikafiri.

Ipo shule nimehusika kuianzisha tangu mwaka 2003 mpaka nikiandika mwezi Februari 2009 bado haijasajiliwa.Kinachozuia isisajiliwe hakiko wazi.Masharti ya kukubaliwa kutoa elimu yamekuwa mengi mpaka yanatisha.

Maana ya elimu ingekuwa kama hivi ilivyozoeleka ,basi wengi wa watu wangepata lawama za kulaumu siku ya kiyama kwa makosa waliyotenda walipokuwa duniani, kwa kusema hawakujua kwa kutokusoma au kwa kukosa gharama kubwa za kulipia masomo au hawakuweza kutekeleza ibada zao kwa vile hawakupata vyeti.

Wapo wasomi miongoni mwa waislamu ambao akili zao ni kali sana katika kuyaangalia mambo yanayotokea katika jamii na kuyachambua.Kwa kuzoea maana ya elimu ya kikafiri basi hupata kiburi kuwa kujua kwao ndio mwisho, na kwamba wengine hawana uwezo wa kuona kama wao.Wanapogundua kuwa wako wenye kujua kama wao huwa hawapendi wenzao hao watoe michango yao ili jamii ifaidike.Nyerere wakati wa EAMWS alipojua kuhusu mpango wa waislamu kujenga chuo kikuu cha mwanzo Tanzania pale Chang’ombe aliingiwa na choyo na kuifisidi mipango hiyo.Tatizo la Nyerere halishangazi kama inavyoshangaza kwa muislamu kuwa na tabia kama hiyo.

Kijiji nilichozaliwa na kukulia kiko mbali sana na mji.Katika utoto wangu na mwanzoni mwa ujana wangu nilihisi ndiko mwisho mwa dunia kwa jinsi nilivyoona ugumu wa mawasilino na sehemu nyengine za ulimwengu.Hivi ninavyoandika watu wa kijijini kwetu tunazungumza na kubadilishana mawazo kirahisi wakati wowote kutokana na maendeleo ya teknolojia ya simu.Wiki hii walikuwa wanaunganisha maji ya mfereji.

Sisi ambao tumeona shida za mawasiliano ndio ambao tunaona maajabu ya maendeleo ya mawasiliano kutokana na fadhila za Mwenyezi Mungu kwa waja wake.Sheikh Muhammed

anakumbuka mwanzoni mwa miaka ya 1990 alipoletewa habari ya kifo kilichotokea nje ya nchi.Ikiwa tayari ni mwezi tangu kifo hicho kitokee bado haikuwa rahisi kuzifikisha habari hizo kijijini zilikotarajiwa kufika.Gharama kubwa iliyotumika kupata gari kupeleka habari hiyo haikufikisha kwenye lengo,kwani walipofika katikati ya safari hawakuweza kuendelea na safari hiyo kutokana na mafuriko yaliyoziba njia.Ikabidi warudi na safari kupangwa siku nyengine.

Hapo zamani sisi ambao hatukuchaguliwa na T.C.U au na mabaraza ya kusajili wanafunzi kuendelea na masomo ya juu, basi kwetu hatuwezi kusoma wala kusema tena.Kwa kutokupitia huko basi hata tukisema hatusikilizwi.Kutokana na fadhila za Mola wetu katika enzi zetu hizi hakuna mwenye uwezo wa kutuzuia kusoma na kusema isipokuwa Allah (s.w).

Hapo zamani elimu ilipokuwa finyu,wakati magazeti na redio ndizo zilizokuwa nyenzo muhimu za mawasiliano na kupeleka habari,watu karibu sote Tanzania tulilazimika kusikiliza redio za taifa na magazeti machache ya serikali.Pamoja na kutokuwa na nyenzo nyengine za kupatia ufafanuzi wa jambo,kuna wakati msomaji au msikilizaji unaumia na kuona dalili za presha na vidonda vya tumbo kwa kusoma au kusikia jambo ambalo unajua ni propaganda na uongo.Mfano ni wakati wa uchaguzi au habari za kuupakazia uislamu na uarabu na biashara ya utumwa.

Baadae watu wakakimbilia redio na magazeti ya kimataifa.Katika siku za karibuni vyombo hivyo vimekuwa vikiongozwa na wasomi wenye vyeti ambao ni zao la mfumo wa elimu wa kikafiri.Habari za mambo ya starehe za kidunia na upuuzi zimekuwa zikiongoza.Hata kwenye vyombo vya habari vinavyoitwa vya kiislamu au vinavyomilikiwa na waislamu utakuta mambo hayo,mara nyengine kulazimishwa na sera zinazovidhibiti.Michango ya baadhi ya watu pia hupigwa na chini na wahariri wanaojali michango iliyoletwa na wenye vyeti.

Wale wenye kuandika mambo ya udaku na umbeya na upotoshaji wa jamii hata tukisema nao ili tuwe pamoja,huwa wanapuuza kwa kujitia uhariri mkali na kuhisi hatuna pa kwenda.Kwa sasa si lazima tuseme nao au tusome habari zao.Mamilioni ya tovuti zimeanzishwa. Nyengine zitasomwa kama zinaandika ya maana na mengine itakufa.

Hii ni nafuu sana kwangu.Ninao uwezo wa kukisia haraka kuwa katika habari fulani nitapata cha maana au ni kupoteza muda tu.Karibuni nimesoma habari ya gazeti Fulani la nchini Marekani lililosita kuchapisha katika karatasi na kuamua kubaki kwenye mtandao tu (online) kwa vile wengi hawanunui tena.Wakati wa matanga ya marehemu baba mwezi Februari 2009.Maeneo yote tuliyopita mjini na vijijini kule Pemba nilishangaa kutosikia sauti ya Zanzibar ikisikilizwa popote,tofauti na miaka iliyopita.Kwa maelezo ya wenyeji inaonesha matangazo ya redio hiyo kwa kiwango kikubwa yanapotea hewani bure.

Ndivyo itakavyokuwa hapo baadae kila mmoja atakapoamua kuandika na kutangaza kwenye tovuti yake bila cheti chochote cha uandishi wa habari kinachodhibitiwa na ukiritimba.Hiyo ni dalili ya kuongezeka na kukuwa kwa elimu.

Kutokana na kuongezeka kwa viwango vya elimu ndio maana hata maadui wa uislamu hawapati tena urahisi wa kuupiga vita uislamu,wasioshiriki katika jihadi hii ni ukosefu wa imani tu,na kutenzwa nguvu na shetani,lakini si kwa kushindwa na mbinu za kivita.Malalamiko ya mataifa 18 yanayopigana na wataliban huko Afghanistan kila siku yanaongezeka.Huu ni ushahidi wa hilo.Teknolojia waliyotaraji kuitumia maadui kwa faida yao haifichiki kwa Taliban na wengine.Katika vita vya Iraq mara kadhaa Marekani imelazimika kukubali habari waliyoipinga kabla juu ya hasara upande wao baada ya ukweli kuoneshwa kwenye mitandao.

Allah (s.w) ni mkarimu mno

Hakika Allah (s.w) ni mkarimu mno,binadamu hawauwezi ukarimu wake.Kama alivyo mkarimu katika elimu,vile vile ni mkarimu mno katika uchumi.

Maendeleo ya kisayansi kutokana na elimu kunamuwezesha mtu kununua chochote popote duniani kwa njia ya *credit card* kupitia *intaneti*.Lakini utashangaa ulipaji wa pesa unawekewa vikwazo na unazuiwa na baadhi ya nchi na mabenki kwa hofu ya kile wanachokiita ugaidi.Nimewekewa vikwazo kulipia bidhaa ninazotaka nchi jirani tu ya Kenya ili hadi kwanza nioneshe *invoice* ya bidhaa hizo ili ijulikane nanunua nini,namlipa nani na pengine ni kodi kiasi gani nilipe kabla hata kupokea hizo bidhaa.

Ukarimu wa namna hiyo binadamu wasiouweeza uko katika elimu vilevile. Wakati kusoma ni jambo lililorahisishwa namna hiyo,wajanja wa kibinadamu wa kuwatoa watu kwenye malengo na faida za elimu wameweka mazonge mengi na vikwazo ili mtu aambiwe kuwa kweli anatoa elimu na ili aitwe kama kweli kapata elimu.Vituo vya kutoa elimu tangu vya uchanga (chekechea) mpaka vyuo vikuu wamefanikiwa kuvidhibiti sawa sawa, mpaka binadamu wenyewe wamekubali kuwa huo tu ndio mfumo halali wa kutoa elimu.

Urasimu huo mbali na kudhibiti akili za watu pia hutoa mwanya mzuri kwa watu wenye vyeti kuwanyonya watu wengine na kujitajirisha kiuharamu.Miaka yote hiyo tangu 2003 kushindwa kupata usajili wa shule ilhali hakuna kosa la wazi ni mfano wa ukiritimba huo wa kutoa elimu.Maeneo yetu yamekaguliwa mara nyingi sana na mamilioni ya fedha yamepotea kwa hatua ambazo naamini ni za kuzuia elimu badala ya kuiendeleza.

Mizozo,migomo na malalmiko yasiyokwisha kwenye vyuo vinavyoitwa vya elimu ya juu ni dalili ya kutofaa mfumo wa elimu tulionao.Ukichanganya na udanganyifu unaolalamikiwa tangu viwango vya chini,naamini utasambaratisha ukiritimba wa elimu duniani kote baada ya miaka si mingi mbele.

Ukomunisti ulikufa mbele ya macho yetu,na ubebari nao uko taabani kwa vile ni mifumo ya kiuchumi na maisha yenye kasoro mbele ya Allah (s.w).Mifumo ya elimu nayo ya kila nchi ambayo imedhibitiwa kimataifa nayo itaishia kufa kama mifumo hiyo ya kiuchumi.

ZANA ZA KUSOMEA CHINI YA MTI

Mwanzoni nilianza kufarijika nilipojua kuwa naweza kufikia mada za maprofesa mbali mbali kupitia intaneti,ambao wangenisomesha chuo kikuu.Wakati nikitafakari masuala ya kielimu nikapata fikra ya kufufua safari yangu ya tangu zamani ya kwenda mwezini.Katika harakati hizo nikagundua kuwa si busara kwenda huko ilhali mwezi bado una matatizo kwa waislamu.Ndipo nikapata fikra ya kuujadili mwezi kwanza, na mambo mengi yanayoungana nao.

Ugumu wa kuujadili mwezi ulianza kupungua niliponunua *Digital Qur'an*,kifaa kidogo cha *elektronik.* Kwa mujibu wa mfanyabiashara na rafiki yangu wa kisomali kina kumbukumbu ya 80GB,hata hivyo nahisi hakina ukubwa wa kumbukumbu hizo.Ndani ina tafsiri ya Qur'an kwa lugha 20 ikiwemo ya Kiswahili na usomaji wake.Ina vitabu karibu vyote mashuhuri vya hadithi.

Baadae nikanunua kompyuta yangu ambayo nilianza kwa kwenda kwenye *internet café* na kurekodi mada nilizohitaji na kurudi kuzisoma nyumbani pole pole kwa kadri wakati ulivlyoniruhusu.

Hayo yote niliona ni maajabu na nikazidisha shukrani kwa Mwenyezi Mungu,lakini kumbe ilikuwa ni mwanzo tu.Katikati ya 2008 nikaunganisha kompyuter yangu na njia ya internet (broad band).Alhamdulillaah,kuanzia hapo huwa naingia maktaba mbali mbali, kubwa kupekua vitabu na mada ninazozihitaji kwa urahisi.Ninao uwezo wa kusoma mihadhara muhimu ya maprofesa wakubwa kutoka nchi mbali mbali.Inapobidi huwa napata vitu vya ziada kwa malipo nafuu.

Mzozo wa mwezi mwandamo kwa maoni yangu ni moja ya eneo lenye kuuaibisha uislamu mpaka wakati wetu huu.Masheikh zetu wengi wana elimu za kutosha na uwezo wa hali ya juu wa kufikiri.Hata hivyo suala la mwezi hawajaweza kulipatia ufumbuzi.Lazima kuna kasoro sehemu fulani ambayo inabidi ipatiwe ufumbuzi.

Siku moja katika mazungumzo na sheikh wangu mmoja nikajaribu kumuelekeza kwenye mtandao fulani wa masuala ya mwezi unaoendeshwa na muislamu mmoja nchini Marekani.Nikamuashiria kuwa kwa kuangalia huko anaweza kuuelewa mwezi vizuri kisayansi.Akaniuliza muislamu huyo ana mustawa gani wa elimu ya kiislamu.Nikajuwa sheikh wangu ameathirika na mfumo wa elimu wa vyeti,nikaamua kutoendelea kujadiliana naye kuhusu suala hili. Badala yake nikaamua kuendeleza kutoa mchango wangu kuhusiana na tatizo hili kwa namna ambayo kwa msaada wa Allah (s.w) iko mikononi mwangu.

Sheikh mwengine alipojua kuwa kuna mtu anajaribu kuipitia mijadala ya mwezi na kuiwasilisha kwa waislamu ili wapime hoja za kila upande,hakupendezewa na hili.Msomi huyu alionesha kuzibeza juhudi hizi na kujisifia yeye kuwa ana uzoefu mkubwa wa mada hii.Kauli yake hii iliashiria kuwa yeye tu ndiye anayestahiki kuzungumzia mjadala huu. Masheikh zetu hawa ni wasomi na watu muhimu sana lakini elimu zao sio kipimo cha elimu yote.

TATIZO LA MWEZI MWANDAMO.

Kutofautiana kwa waislamu kuhusu mwandamo wa mwezi na tarehe zao ni tatizo sugu na la miaka mingi na hata karne nyingi. Wanazuoni wetu wanalirudisha nyuma tatizo hili tangu mara tu Mtume(S.A.W) alipoiaga dunia. Wengine wanasema baada ya miaka 30 tangu kufariki kwake, wakati wa utawala wa Muawiya (R.A).

Makongamano mengi yamefanyika kujaribu kuleta ufumbuzi lakini bila mafanikio. Historia inaonyesha kuwa makongamano hayo yamekuwa yakifanyika nchi mbalimbali duniani bali hata katika miji tofauti ndani ya nchi.

Waswahili wana msemo usemao kila anayelia hushika kichwa chake. Hili tatizo la mwezi mwanadamu linaonesha ni bay. Zaidi kwa nchi za Afrika Mashariki na hasa Tanzania. Katika miji ya Tanzania, atyhari imekuwa mbaya zaidi kwenye mji wa Tanga, ambao una taasisi nyingi za Kiislamu na wasomi wengi wa fani mbalimbali.

Katika jiji la Tanga ni kawaida sana kuwa na sikukuu mbili. Leo unaona waislmu wamevalia vizuri wanakwenda kusali Idi viwanja vya Tangamano. Kesho yake wengine wamevalia vizuri wakitoka misikiti mbalimbali baada ya kusali Idi nytengine. Kumekuw ana ufahamu tofauti wa aya za Qur'an na hadithi zinazohusiana na kuanza na kumaliza kwa mwezi. Hasa kwa mwezi wa Ramadhani ambao ufuatiliwaji wake kutoka wa waumini wa kiislamu ni wa kipekee. Hili nimelishuhudia binafsi kwa kipindi cha miaka takriban 20 ambayo mimi nimekuwa miongoni mwa wafuatiliaji wa karibu.

Makongamano ambayo yamekuwa yakifanyika miji na nchi mbali mbali yamekuwa yakihudhuriwa na kuchangiwa na wasomi wakubwa wa fani tofauti. Hoja nzito zimekuwa zikitolewa. La kushangaza ni kuwa hali ya kutofautiana kwa waislamu kuhusu tarehe zao ndio imezidi kuwa mbaya.

Walimu na watu wa *Usulu Da'awa* wanapaswa kufanya tathmini ya somo hili, ili kujua sehemu ambayo haijaeleweka vyema ili watumie mbinu tofauti kuielezea. Kwa walimu ni jambo la kwaida kubakili njia za kulifahamisha somo kila tathmini yake inavyoonesha wanafunzi wake hawakuelewa kwa njia iliyotangulia. Isingekuwa haraka za kumaliza mihutasari na kozi zilizopangwa ili kuwahi mitihani, basi ni wanfunzi wachache sana wangeshindwa kuelewa jambo gunia, baada ya njia zote za kulifahamisha somo kutumika.

Kwa somo la mwezi, kingehitajika kutumia mbinu zote za kiuwalimu ili waislamu waelewe na kueleawana, jambo ambalo ni hitajio la kidharura kwa dini yao.

Nikiwa ni msomi na mwanafunzi wa chini ya mti wa fani ya uwalimu wala sijatia nia ya kuifanya kazi hiyo, na nimejijua kuwa kazi hiyo ni kubwa mno kwa hali yangu, na sina sifa za kujitwisha mzigo huo. Hata hivyo katika matayarisho ya safari kwenda mwezini kwa kufuatana na kikundi cha masheikh, nahisi kama kwamba nimepata maelezo mengine ya kuieleza siku ya kiislam kwa kutumia mawimbi ya bahari.

Nimeshawishika hivyo kwa kuzipitia takwimu za maji kupwa na maji kujaa, ambazo bila shaka waliozitayarisha hawakukusudia zifanye kazi hiyo. Kwa vile ni takwimu kutokana na

maumbile ya Mwenyezi Mungu zinaweza zikawa na kila aina ya ujumbe ambao umejificha kwao.

Rafiki yangu wa tangu utotoni na ndugu yangu wa kifamilia katikati ya Januari 2006, tarehe 13, alikuja nyumbani kunitembelea. Kama kawaida ya mazungumzo yanavyozunguka huku na kule, mwishowe tukaja kwenye mada ya waislamu na matatizo yao. Hapo tukagusuia jinsi wanavyokosa umoja kupambana na adui zao, baada kya kila mmoja kutoa mifano yake; Iraq, Afghanistan, Chechniya tukafika kwenye suala la mwezi. Akanikatisha mazungumzo kwa suali " Samahani mwalimu, nikukatishe, Hivi wewe uko upande gani?, wa Bakwata au wa Ansaar ?".Ni swali maarufu wanaloulizana waislamu miaka hii wanapogusia mzozo wa mwezi.

Ni kweli mimi nilikuwa upande mmoja kati ya hiyo lakini sikuuweka wazi. Pamoja na hivyo nimegundua kuwa upande wangu nao hauna jibu la moja kwa moja , kama tutakavyoona mbele.

Siku ya tarehe 30- 12- 2006 nyakadti za alfajiri ambapo nilimaliza majaribio ya awali ya takwimu za maji kupwa na maji kujaa, ilikuwa ndio muda ambao ulitajwa kuwa Saddam Hussein, aliyekuwa Rais wa Iraq angenyongwa.

Vyombo vya habari hasa vya kimagharibi na vya Serikali kibaraka ya Iraq vilikuwa vinawataarisha wasikilizaji na watazamaji wao kuzipokea habari hizo kwa wema wa aina yao. Vilikuwa vinajaribu kupunguza manun'guniko, pengine kwa kuondosha uwezekano wa kutokea fujo zaidi. Mpaka wakati hou juhudi zao zote za kuzima machafuko waliyoyaanzisha zilikuwa zimeshindikana. Hali hiyo ilikuwa inaendana na kauli ya balozi wa Marekani Iraq, bw, Khalilazad aliyoitoa kabla, kwamba Marekani nchini Iraq ni kama kwamba wamefungua "Pandora box" msemo wenye maana kuwa madudu yaliyofumuka kutoka boksi hilo imekuwa tabu kuyarudisha na kuyafungia ili yasiendelee kuleta tabu.

Kwa shinikizo la Marekani ili kuwahi kutekeleza ajenda za Bush ambazo alikwishaziahidi mapema mwezi huo. Kwamba angetangaza mpango mpya wa Iraq kabla ya mwesho wa mwaka. Na kwa kukosa heshima kwa dini ya kiislamu walikuwa wamesahau utukufu wa siku hiyo, na kusahau uovu wa ziada wa kuunganisha na kuendeleza dhulma ya kumuua kiongozi wa watu, ndani ya siku tukufu, siku ambayo pia inajulikana kwa jina la siku ya kuchinja.

Siku ya nyuma yake waislamu walikuwa wamesimama Arafa kwa Ibada kya Hija mwaka 1427. hivyo siku ile ilikuwa ni sikukuu kwa baadhi ya waislamu na wengine wao ilikuwa ni siku iliyofuata. Vyombo hivyo vya hyabari vilikuwa vinashangiria tarehe mbili za kiislam ndani ya siku moja katika mji mmoja. Kwa wale wa kishia, siku hiyo ilikuwa ndiyo Arafa yenyewe kwa sunni ndiyo Idi ya Kuchinja na cha kuchinjwa hakikusudiwa kiwe mtu bali ni mnyama.

Baadhi ya vyombo hivyo vilikuwa vikijutia kibri cha Marekani kwa kuchagua kumnyonga Saddam aliyewekwa kwenye kundi la masunni ambayo siku hiyo ilikuwa ndiyo sikukuu yao ya kuchinja.

Kiongozi wa jopo la mawakili lililokuwa likimtetea Saddam, wakili wa kimataifa Najjiib Al Nuaim alikuwa ameakata tama na utetezi wake na tayari alikwisharudi kwao Qattar. Mambo ya Saddam alikuwa akiyauliza na kuyajibu kwa simu na video tu. Alisema kunyongwa kwa Saddam kulikokuwa kukisubiriwa wakati wowote si jambo la utani na kwamba halikuwa na uhusiano wowote na hukumu ya kisheria bali ilikuwa ni mchezo wa kuigiza wa kisiasa kulingana na matakwa ya Marekani.

Bwana Najib alifafanua kuwa serikali, majaji waliokuwa wakisimamia kesi hiyo vilikuwa ni vyombo vya kimarekani. Hata ushahidi uliowasilishwa mahakamani wa kumtia hatiani Saddam ulitolewa na vyombo vya kimarekani.

Kweli ilipofika saa 12:05 walimnyonga Saddam Hussein. Ilikuwa ni siku nyengine ya huzuni na aibu kwa waislamu. Udhaifu wa tarehe za kiislamu uliwafanya mashia wa Irak wajione ni watu tofauti na Massuni. Hivyo ndivyo ilivyokuwa ikipambwa na maadui wa Uislamu ambao daima huwa wanatumia fursa za tofauti za waislamu ambazo huwa wanazijua eneo kwa eneo kuzidi kuwapiga waislamu.

Mashia wa Marekani tayari walikuwa wamekushanywa kushangilia kifo cha Saddam Hussein. Kwao sikukuu, siku ya pili yake ilifanywa ionekane ni sikukuu mbili kwa pamoja ya kuchinja na ya kuchinjwa kwa Saddam Hussein aliyeoneshwa kuwa ndiye adui yao mkuu na pekee duniani.
Pamoja na huzuni ya kudhulumiwa Saddam na kejeli kwa tarehe za kiislamu, nilifarijika kuwa maelezo mengine ya kuieleza siku ya kiislamu niliyokuwa nayo yangesaidia kuondosha au kupunguza aibu hii ya tofauti hizi zinazovunja umoja wa waislamu.

Haiwezekani kwa dini ya kiislamu, dini ya kimaumbile na dini ya sayansi, iwe na udhaifu wa kuwa na tarehe mbili mbili. Ni uhakika wa asilimia mia moja; kuwa siku ya kiislamu na tarehe za kiislamu ni moja moja tu kwa dunia nzima. Kwa upande mwengine haiwezekani kuwa siku hiyo na tarehe hizo hazina maelezo mengine ya kuonesha umoja wake, na kwamba tatizo hilo ni la milele kwa waislamu.

Sijui maelezo yangu mengine ya siku hiyo kwa mawimbi ya bahari yatakubalika kwa asilimia ngapi, hata rafiki na ndugu yangu aliyekuja kunitembelea nyumbani na kumdokeza habari hii alicheka sana na kunipa ushauri wa kihekima.Baada ya kumaliza kucheka akasema atakaporudi nyumbani kwake Dar es Salaam angeulizwa *Tanga kunani?* [1],angekuwa na vitu viwili vya kuhadithia ambavyo alivisikia na kuvishuhudia.Moja ya vitu hivyo ni kuwa kuna mtu ana jawabu ya mzozo wa mwezi.

Baada ya kuridhika na binafsi na maelezo yangu na kama kwamba nataka kuanzisha mjadala mpya wa mwezi,nimelazimika kufuatilia mijadala na makongamano yaliyotangulia kuhusiana na mada hii.Madhumuni ya mwanzo ya uamuzi huo ni kupata uelewa mpana wa suala ninalotaka kushiriki kulitolea maelezo.Vile vile kuona iwapo jambo ninalotaka kulifafanua jee limewahi kujadiliwa?.Iwapo tayari nilinganishe yale niliynayo nay a wenzangu yanakubaliana kiasi gani,na wapi pa kuwekewa mkazo.Hata hivyo kama

tutakavyoona mbele mpaka naanza kuratibu mijadala hii hakuna sehemu ambapo maelezo haya yametangulia kimaandishi, kwa angalau yale niliyoyafikia.

Nimepekuwa kwenya mitandao mbali mbali (web search),kuona mwezi mwandamo ulivyohusishwa na mawimbi ya bahari.Nimepata makala nyingi za mada ya mwandamo wa mwezi ,na nyingi zenye kutaja mawimbi kwa takwimu tofauti za kitafiti za kisayansi.Hata hivyo mpaka tarehe 17/02/2007 na sasa 30/10/2008 sikupata maelezo yoyote yenye kuhusisha vitu hivi, na kuonesha kuwa ni nyenzo ya kutoa ufumbuzi wa mwezi.

Hii yaweza ikawa na maana mbili.Ama maelezo yangu hayakubaliki ndio maana wasomi waliobobea hawajaona umuhimu wa kuyawasilisha.Vyenginevyo ni maelezo mapya hakuna aliyeyaandika,jambo ambalo pia si ajabu, kwani elimu haina mwisho na kufikiri,kuwaza na kupanga ni haki ya kila binaadamu wa kila enzi.

Kama ilivyo kawaida kwa hamu ya kuona na kusikia jambo jipya ,najua wasomaji tayari wanaanza kurusha mikono hewani na kufoka.Ni maelezo gani mapya hayo!. Wanahisi nawazungusha na kuwapotezea muda wao. Kundi hili dogo kimaumbile ya mkusanyiko wa watu, nalishauri liwe na uvumilivu na kufuatilia mijadala hiyo hatua kwa hatua,kwani bila hivyo sitoweza kueleweka na hatutafahamiana.

Kabla kuja kwenye mjadala wa mwezi kwa mawimbi ya bahari tutaangalia mijadala minne ya mwezi. Mitatu ya hapa nchini, na mmoja nje ya nchi. Mijadala yenyewe ni (i) Semina ya Kiislamu iliyofanyika kwenye ukumbi wa EACROTANAL ZANZIBAR tarehe 22/05/ 1991 – 23 – 05 -1991 (ii) Majadiliano ya kielimu – Kengeja , Pemba tarehe 19 /03/1995 (iii) Kongamano kuhusu kuandama mwezi – Njuweni Hotel, Kibaha tarehe 5/3/1998 na (iv) Conference on Hilal Sighting, organized by Fiqh Council of North America (FCNA)' tarehe 10/6/2006; Virginia – Marekani.Mjadala huu utawakilisha mijadala mbali mbali ya kimataifa na ya kisayansi inayohusiana na mwezi.

Katika mijadala hiyo nimesikia mara mbili tu, kauli zenye kuashiria bahari, Moja ni msemo wa watu wa pwani usemao "Ni yayo kwa yayo maji ya futi na nyayo nyengine ni pale mmoja ya watoa mada alipotaja mabadiliko ya hali za mwezi yanavyosaidia uvuvi wa samaki aina ya vibua kama ilivyotajwa kwenye mjadala wa Unguja.

1.*Msemo maarufu wa utani kutokana na mazungumzo ya watu wa Tanga*

Nitapendelea wasomaji kwa uvumilivu mkubwa wafuatilie hoja za kile upande za mada hii kwenye mijadala hiyo kwa kadri Allah (s.w) atakavyotuwezesha Tutazinakili hoja hizo kwa uadilifu kadri itakavyowekanaa.Wasomaji wataweza kufahamu wapi kasoro ilipo na kuja kuufahamu mjadala wa mwezi kwa mawimbi utakaofuatia baada ya mijadala hii.Ikiwa haitosaidia, basi tutakuwa tumeongeza faida ya gharama na muda vilivyotumika kuviandaa vitu hivyo.

Kutokana na upana wa Elimu ambayo ni milki ya Allah (S.W) wakati tukifuatilia mihutasari ya mijadala hiyo iliyotangulia, nawaomba wasomaji walioona popote kwenye vitabu walivyonavyo au waliosoma kwenye mitandao mbalimbali ya intaneti basi wanishauri kuhusu mada hii.

Kabla ya kuanza mfululizo wa mijadala yetu ya mwezi, itabidi tutoe majina ya pande mbili .zinazojadiliana

Kwa kuzingatia mazoea ya majina yanayotumiwa sana na waislamu Tanzania, na kwa kuzingatia mjadala wa mwiso tutakaoutolea muhtasari wake; tutakuwa na upande wa Bakwata na upande wa Ansaar Suna. Haya ndio majina yaliyotumika na ndiyo makundi mawili yaliyoshiriki kwenye mjadala wa Kibaha wa 1998, ambao ndio wa mwisho .kuujadili kwa mijadala ya hapa nchini

Wengine walioshiriki kwenye mijadala hiyo na watakaoshiriki si wafuasi wa kundi lolote .katika haya, lakini bado itabidi wagawike na kuwaita katika moja ya pande hizo

Kwa mfano washiriki wa mjadala wa Eacrotanal, Zanzibar wako waliotoka nje ya Tanzania, hasa Kenya ambako hakuna Bakwata , lakini sisi tutawagawa wenye hoja za kiansari na wenye hoja za Bakwata. Mjadala wa Marekani, nako tutakutana na wenye hoja za Ansari na wenye hoja za kibakwata

Mimi mwenyewe mpaka tutakapoanza mjadawa wa mwezi kwa mawimbi ya bahari, naomba nichukuliwe kuwa si mfuasi wa kundi lolote katika hayo. Hata hivyo mjadala .utakapoanza naamini wasomaji wataweza kutoa jina na kusema ni mjadala wa aina gani